Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na katika watu wako wanaoshika washirika kinyume cha Mwenyezi Mungu, wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana; ...
(*Al- Baqara*) (2:166).

JUZU 74 No. 179 | JAMAD I/JAMAD II 1435 AH | APRIL 2014 | SHAHADAT 1393 HS | BEI TSH. 500/=

Khalifa Mtukufu awaambia Waahmadiyya:

Jitahidini kupata Mapenzi ya Mungu

Na Mwandishi wetu

Katika moja ya hotuba yake ya Ijumaa, Kiongozi wa Waaminio dunia Khalifatul Masih V a.t.b.a. Hadhrat Mirza Masroor Ahmad alitoa hotuba, akinukuu maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliyoelezea juu ya Mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Khalifa Mtukufu akasema katika maandishi haya Mapenzi ya Mwenyezi Mungu yanafafanuliwa kwa kina na maana yake pia inaelezewa pamoja na siri ya jinsi ya kuyafikia na pia hekima yake inaelezewa. Pia maandishi yanaelezea ni kipi kinatakiwa kiwe kiwango chetu, sisi tuliomkubali na kujiunga na Jamaat yake kuhusiana na



Masjid Baitul Futuh (Nyumba ya ushindi) jijini London ambako hotuba hii ilitolewa

Mapenzi ya Mwenyezi Mungu, na pia ni kipi ambacho Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa anakitegemea kutoka kwetu. Kila nukuu ina ufasaha mkubwa na maana pana na hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kuizingatia ili tupate kuelewa maana yake na roho ya ujumbe uliomo na hivyo tupate kuufuata na kuweza kujirekebisha.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema: Mapenzi si jambo la kuigiza kwa matendo fulani ya juu juu tu, bali ni kipawa maalum miongoni mwa vipawa vya mwanadamu. Uhalisia wake ni kwamba

Endelea uk. 3

Sheikh K. Amri Abedi Atunukiwa Nishani ya kumbukumbu ya miaka 50 ya muungano

Na Mwandishi wetu

Mnamo majira ya jioni ya tarehe 2 April, 2014, ukumbi wa mikutano wa ndani ya Ikulu ulikuwa umefurika wageni waheshimiwa waliojawa bashasha na shauku, wakiisubiri saa makhsusi ambapo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, awasili ukumbini na kukabidhi Nishani na tuzo makhsus kwa wateuliwa 86 waliobahatika kutunukiwa tuzo hizo katika kuadhimisha sherehe za miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, muungano uliounda nchi ya Tanzania, jina lililoasisiwa na Bwana Muhammad Iqbal Dar, mwanajumuiya wa Ahmadiyya aliyekuwa mwanafunzi wa shule ya Mzumbe Morogoro, mnamo mwaka 1964, kama alivyosema mwenyewe kwamba Tan iliwakilisha Tanganyika, Zan iliwakilisha Zanzibar, I iliwakilisha jina lake Iqbal (lenye maana ya kukubalika mbinguni) na herufi ya mwisho ya A ikiwasilisha Ahmadiyya katika kutafuta msaada wa Mwenyezi Mungu katika kuupata ushindi wa ubunifu wa jina hilo na Mungu Akaufanikisha ushindi huo.

Mama Maria Nyerere alikuwa amewasili mapema tu na kuketi kwenye kiti chake mnamo safu ya kwanza. Punde mama Karume naye aliingia ndani ya ukumbi huo uliokuwa ukivuma muziki wa bendi ya Polisi iliyokuwa ikitumbuiza kwa hatua. Mama Karume aliketi pembeni ya mjane wa Mwalimu Nyerere bi Maria.

Kila mara watu wenye hadhi na taadhima walikuwa wakiingia ukumbini humo mmoja baada ya mwingine, Brigedia Jenerali Ramadhani haji Faki, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mh. Hamid Ameir Ali, Mheshimiwa Clement George Kahama, Mh. Job Malecela Lusinde, n.k. waliendelea kuingia ukumbini na huku sauti tofauti zikisikika,



Marehemu Sheikh Kaluta Amri Abedi aliyekuwa Meya wa kwanza Mwafrika wa jiji la Dar es Salaam, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Waziri wa Sheria na Waziri wa utamaduni na maendeleo ya Jamii

zilizokuwa zikiandamana na vicheko vya wapendanao waliokutanishwa humo baada ya miongo kadhaa.

Mama Saidi Maswanya aliingia taratibu kwa mwendo wa hatua za kuhesabu, akiongozana na bintiye Rose Maswanya, Mwanawe Kululinda na mjukuu wake wa kike waliokuwa wakimsaidia kumtembeza.

Karatasi zenye majina ya watunukiwa ziliwekwa juu ya kiti cha kila mhusika.

Mheshimiwa Rais alikawia kuwasili na ilipofika saa mbili ya usiku, zikaanza kuonekana pilika pilika zisizo za kawaida toka kwa waandalizi wa hafla hiyo maalum.

Punde wakaanza kuingia waheshimiwa wa ngazi za juu wakiwemo Marais wastaafu wa Zanzibar Mh. Abedi Amani Karume na Mh. Salmin Amour, Cleopa David Msuya, Joseph Sinde Warioba, Salim Ahmed Salim, Dr, Shein, Dr.

Endelea uk. 7

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

JE TUNAWEZA KUHALALISHA MATESO?

Taasisi nyingi za kutetea haki za binadamu, vyuo vikuu na magazeti nchini Marekani na Ulaya vyombo vyote hivyo kwa hivi sasa vinashughulikia dhana nzima ya mateso. Swali linalowasumbua; Je kuna uwezekano wa kuwepo sababu yoyote iwayo inayoweza kulazimisha jamii katika utumiaji wa mateso ili kupata taarifa au kumkomoa mtu?

Mtindo huo unatumika sana sehemu nyingi duniani kwa hivi sasa. Mateso tunayoyasikia yaliyowasibu hao waliyokutana nayo ni ya kuogofya na kufanya nywele zisimame kichwani. Yaliyotokea huko Gwantanamo Bay nchini Cuba yanaonesha kwa kiasi gani sehemu ya unyama katika binadamu inavyoweza kujitokeza. Islam inapinga kwa nguvu zake zote mtindo huo wa kutumia mateso kwa njia yoyote iwayo.

Nchi za Magharibi zinaamini katika kanuni za Demokrasia zimo katika kizungumkuti kikubwa, unawezaje kupambana na magaidi na bado ukaendelea kutekeleza mila na desturi za Demokrasia zinazopinga mateso?

Marekani ndio hasa iko njia panda, kwani ndiyo imejitia kimbelembele kuwa polisi wa dunia, na kutuliza fujo, kuwabwatukia wengine lakini maskini inashindwa kuondoa boriti katika jicho lake na kukimbilia kutoa vibanzi katika macho ya wengine.

Hapo ndipo heshima ya Marekani inapoporomoka mithili ya nyumba ya karata. Inaamuru kutenda mema na wanasahau nafsi zao. Na hilo kwa hakika ni chukizo kubwa kusema usiyoyatenda.

Wakati taifa la Marekani na mataifa mengine yakiwa kwenye mahangaiko ni jambo la busara kufahamu Islam inasemaje kuhusu mateso na dawa ipi inayotakiwa itumiwe.

Islam inalaani mateso na inasisitiza ya kuwa kifo ni afadhali kuliko mateso. Mateso maana yake ni kwamba kufa hufi lakini cha moto unakipata. Lakini Islam inasemaje juu ya mateso kwa ujumla? Aliyeleta ufafanuzi uliokamilika na usio na shaka ndani yake kuhusu mafunzo ya Islam ni Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Muujiza mkubwa wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ni kwamba alibadili maneno yote yaliyo katika Qurani Tukufu na kuyapa sura ya vitendo. Na kama sote tunavyofahamu mafunzo ya Islam yote yamo katika Qurani Tukufu. Kama alivyosema Bi. Aisha (ra) alipoulizwa juu ya maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alijibu kwa neno moja 'Qurani Tukufu'.

Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alikuwa na roho ya upole, huruma iliyojaa maziwa ya upendo. Kuonea watu ni jambo lililomuumiza sana. Akiwa kijana mbichi alijiunga na kundi lililokuwa linatetea wanyonge. Hadhrat Abbasi alifungwa kwa kamba, maumivu yake yalimfanya atoe sauti ya maumivu na Masahaba wakaona walegeze kidogo kamba. Mtume (saw) akauliza; "Mbona sisikii sauti ya Hadhrat Abbas?". Wakasema wamelegeza kamba. Hivyo akawaamuru wafanye hivyo kwa wote. Waongoza majeshi wa Kiislam walipewa maagizo maalum ya kutowagusa wazee, watoto, akina mama na wasio katika mapambano. Mahekalu na Masinagogi iliamuriwa yasiguswe. Miili ya waliouawa haikuruhusiwa kuguswa kwa nia ya kuiharibu.

Picha hii inatupa taswira ya Islam inavyoona mateso. Ni jambo halikubaliki hata kidogo kuwatesa binadamu. Kuna mengi sana ya kujifunza kutoka katika Islam. Vyanzo vyote vya chuki na uhasama vimezuiliwa na Islam. Njia pekee ya kuzibua vyanzo hivyo ili maji ya uzima ya Islam yapite ni kumfuata mbora wa viumbe wote, sababu ya kuumbwa dunia, Siraajul Muniir, Nabii mwenye daraja Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Kinyume cha hivyo ni kuendelea na mateso ambayo yanaonekana hivi sasa duniani.

Malfudhaat Sayedna Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Mnamo mwaka 1895, Bwana Mufti Muhammad Swadiq Sahib anaandika ya kwamba mwaka 1895 wakati nilipokuwa nikimhudhuria kwa Hadhrat Ahmad as, basi kutokana na shauku yangu niliyokuwa nayo wakati ule, nilikuwa nikiandika maneno yake matakatifu kwenye karatasi na kwenda Lahore na huko nilikuwa nikiwasomea wanajumuiya katika kikao kilichokuwa kinafanywa kila wiki. Kutoka kumbukumbu zile baadhi ya mazungumzo ya Seyydna Ahmad as yanaandikwa hapa.

BAIAT NA TOBA.

Seyydna Ahmad as alisema, inapaswa kueleweka ya kuwa katika kufanya baiat mna faida gani na kwanini hii inahitajika? Maadamu faida na thamani ya kitu isipoeleweka, heshima yake kitu hicho haishiki nafasi machoni mwa binadamu kama ambavyo nyumbani mwa mtu vitu vya aina aina vinapatikana, kwa mfano hela, fedha, mbao na kadhalika, basi vitu hivyo vinatunzwa sawa na thamani yake, yaani mwenye nyumba hatafanya mpango wa kutunza mbao kama vile atakavyotunza hela na fedha bali mbao ataziweka tu kwenye kona moja ya nyumba, vivyo hivyo atavihifadhi zaidi vitu vile ambavyo vikiharibika vinaweza kumletea hasara zaidi, vivyo hivyo katika kufanya baiat kuna jambo kubwa sana ambalo ni toba ambayo maana yake ni kurejea.Toba au kutubu ni jina la hali ile ambapo binadamu anaacha na kuaga madhambi yake yote ambayo anakuwa na mahusiano makubwa nayo kana kwamba yamekuwa makazi yake na nchi yake na maana ya kurejea ni kushika utakaso. Sasa kuiacha nchi ni kitu kikubwa sana na kunaleta matatizo mengi, binadamu anapoaga nyumba yake, basi kwa kiasi gani anapata shida? na wakati wa kuiacha nchi analazimika kuwaacha marafiki zake wote na kwa kuviacha vitu vyote kama vile vitu vya nyumbani, majirani, mitaa na masoko analazimika kuhamia katika nchi nyingine na harudi tena kamwe, hii ndiyo toba.Marafiki wa uasi ni wengine na marafiki wa uchaMungu ni wengine, mabadiliko hayo yameelezwa na masufi kwa jina la mauti. Anayetubu analazimika kuvumilia matatizo mengi na wakati wa kutubu toba kweli mabalaa makubwa makubwa yanatokea mbele yake, na Mwenyezi Mungu ni Mrehemevu, Mkarimu.Yeye Hampi mauti mtu huyo mpaka Ampatie mbadala wake. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda wanaotubu, ndani yake mna ishara hii ya kwamba binadamu kwa kufanya toba huwa maskini asiyekuwa na kitu chochote, hivyo Mwenyezi Mungu Anampenda na kumwingiza kwenye kundi la watu wema. Mataifa mengine hayamfahamu Mungu kuwa Mrehemevu, Mkarimu. Wakristo walimfanya Mungu kuwa mdhalimu na mwanaye kuwa mrehemevu yaani baba hakuwa tayari kuyasamehe madhambi lakini mwanaye alitoa nafsi yake kwa ajili ya kupata msamaha. Huu ni ujinga mkubwa sana wa kuweka tofauti kubwa kati ya baba na mwanaye. Baba na mwanaye hufanana katika tabia na khulka lakini hapa sifa hii haipo kabisa. Kama MwenyeziMunguAsingekuwa Mrehemevu basi binadamu asingeweza kuendelea kamwe. Yule Ambaye Alitengeneza vitu vingi sana kwa ajili ya binadamu je tunaweza kutafakari ya kwamba hatakubali toba na matendo mema?

Seyydna Ahmad as anasema; kufanya baiat kwa ulimi tu hakuleti faida yoyote, wanafiki walikosa imani kwa sababu ya kutokuwa na mahusiano kweli na Mtukufu Mtume saw, hawakuweza kuonesha mapenzi kweli na ikhilasi, hivyo kusoma LA ILAHA ILLALLAH kwa ulimi hakuwaletea faida yoyote. Basi mahusiano yanapaswa yaongezwe, kama binadamu haongezi mahusiano yake na Allah na hajitahidi kwa ajili yake basi kulalamika na kuhuzunika kwake ni bure tu. Mahusiano ya mapenzi na ikhilasiyanatakiwayaongezwe, binadamu anapaswa kuelekea upande wa ukweli na ibada na ajikague kuanzia asubuhi hadi jioni.

Msisitizo juu ya Tahajjudi. Seyydna Ahmad as anasema, kama muda wote ukipita katika kushughulika mambo ya dunia basi kwa ajili ya akhera ni kitu gani kimewekwa kama akiba?

Amkeni kwa ajili ya sala ya tahajjudi kwa shauku na mapenzi na kuisali kwa ikhilasi, inaweza kutokea kasoro katika sala zingine kwa sababu ya kazi, Mwenyezi Mungu Ndiye Anayetoa riziki, mnapaswa kusali sala kwa wakati wake. Watu watakatifu na wema waliopita duniani, wale ambao walikuwa wakiamka usiku na kusimama usiku kucha katika ibada mpaka asubuhi, je mnafahamu ya kuwa hao walikuwa wana nguvu nyingi za mwili, hapana. Kumbukeni ya kwamba nguvu ya mwili haiwezi kufanya kazi ile ambayo inaweza kufanywa na nguvu ya kiroho. Mtakuwa mmeona watu wengi ambao wanakula mara tatu au mara nne kwa siku na wanakula vyakula vinono lakini matokeo yake yakawa haya ya kuwa mpaka asubuhi wanaendelea kusinzia na usingizi unawatawala mpaka wanashindwa kufanya kazi yoyote kwa sababu ya usingizi na uzembe wao, hata hivyo wanaona taabu katika kusali sala ya isha, achilia mbali sala ya tahajjudi.

Angalieni masahaba wa Mtukufu Mtume Muhammad saw, je walikuwa wakipenda starehe na vyakula vinono, hapana. Katika vitabu vya zamani imeandikwa hivi ya kuwa hao watakuwa wakisimama usiku na kufunga saumu mchana, muda wao wa usiku ulikuwa ukipita katika kumkumbuka Allah, maisha yao yalipita kivipi? Kurani Tukufu inaeleza hali ya maisha yao katika aya ifuatayo, na kwa kufunga farasi mipakani, ili kwazo mwogofishe adui za Mwenyezi Mungu na adui zenu na enyi mlioamini, subirini na subirisheni, na kuweni imara, na mcheni Allah ili mpate kufaulu. Mwenyezi Mungu Atujaalie kutekeleza hayo yote katika maisha yetu,amin.

Mfasiri: -Sheikh Waseem Ahmad khan Tabora

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo
Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Jitahidini kupata Mapenzi ya Mungu

Kutoka uk. 1

moyo hupendezwa na jambo fulani na kisha huvutiwa nalo. Kama vile ambavyo sifa za kitu hudhihirika kinapofikia ukamilifu wake, basi ndivyo hivyo pia yalivyo mapenzi. Hazina zake huwa bayana yanapofikia kilele cha ukamilifu. Mwenyezi Mungu anasema:

Na wakanyweshwa mioyoni mwao (mapenzi ya) ndama kwa kufuru yao. (2:94).

Kwa hakika mtu anapompenda mwingine ni kama vile anakuwa amemmeza au amemjaza ndani mwake na anakuwa anamuigiza kwa kila tabia na tendo lake. Kadri mapenzi yanavyokuwa makubwa, ndivyo hivyo pia kiasili mtu anapokuwa karibu zaidi na anayempenda kiasi hiki kwamba hufikia hali ya kuwa picha ya mtu huyo. Hivi ndivyo pia inavyokuwa mtu ampendapo Mwenyezi Mungu, Hupata nuru ya Mwenyezi Mungu kwa kiwango sambamba na kiwango cha Mapenzi yake. Na pia wale wanaompenda shetani nao huzungukwa na kiza kilichomo ndani ya shetani. (Nur ul Haq, Part II, p. 430, Ruhani Khaza'in Vol. 9).

Huzur akaelezea kwamba kuigiza sifa za Mungu ni ishara ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kama vile alivyokwisha elezea kwenye hotuba zake zilizopita kuhusiana na utambuzi au uelewa wa Mwenyezi Mungu wiki chache zilizopita; kwamba bila ya kuwa na utambuzi juu ya sifa za Mwenyezi Mungu, mtu hawezi kamwe kumwelewa na kumfahamu. Mapenzi ya Mwenyezi Mungu ni hatua ya juu zaidi, na mtu anapojipaka rangi/sifa za Mwenyezi Mungu ni hapo tu ndipo anapopokea nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Uhalisia wa mapenzi ya kweli unashurutisha kwamba mtu kwa ukweli kabisa azipende sifa zote, tabia zote na kumheshimu sana yule anayempenda na kisha ni lazima ajitahidi mwisho wa jitihada zake kuziigiza hizo kiasi hiki kwamba azame ndani yake, na hapo tu ndipo anapoweza kuyafikia maisha ya mpendwa wake. Yule aliye ni mpendaji wa kweli hujitolea wote kwa ajili ya mpendwa wake na muda wote huwa tayari kukidhi matakwa ya mpedwa wake na moyoni mwake mnakuwa na alama maalum kwa ajili mpendwa wake. Ni kana kwamba mpendwa wake anatembea ndanimwe. Huzama ndani ya mpendwa wake hadi huwa bayana kwa watu kwamba yeye amezama moja moja ndani ya mpezi wake.

Akijibu shutuma iliyoletwa na padri mmoja kwamba



Masjid Baitul Futuh (Nyumba ya ushindi) jijini London ambamo Hadhrat Khalifatul Masih hutoa hotuba zake za Ijumaa

Islam haifundishi kumpenda Mwenyezi Mungu, Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliandika: Basi ieleweke wazi kwamba shutuma hii inaihusu hasa Injili na sio Quran kwa sababu Biblia haifundishi kuwa na Mapenzi binafsi na Mwenyezi Mungu. Quran tukufu imajaa mafundisho haya. Quran tukufu inafundisha:

Na mwishapo kuzitimiza ibada zenu (za Haji), basi Mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama mnavyowakumbuka baba zenu au kumbukeni zaidi; (2:201).

Na katika watu wako wanaoshika washirika kinyume cha Mwenyezi Mungu, wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana; (2:166).

Yaani kwamba mpendeni Mwenyezi Mungu zaidi kuliko muwapendavyo baba zenu, na hiki bila shaka ni kitambulishi maalum cha waaminio kwamba wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi kuliko kila kitu. Hawapendi baba zao, mama zao na wapendwa wao wengine zaidi ya wampendavyo Mwenyezi Mungu.

Kisha inasemwa kwamba: Lakini Mwenyezi Mungu Ameipendezesha kwenu imani, na Ameipamba mioyoni mwenu, na Amewafanyeni mchukie ukafiri na ufasiki na uasi. Hao ndio walioongoka, (49:8).

Na pia inasemwa: Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anaamuru uadilifu, na hisani, na kuwapa (watu kama uwapavyo) ndugu; na Anakataza upujufu, na uovu, na uasi. Anawanasihini ili mpate kufahamu. (16:91).

Aya hii inaelezea haki za Allah na haki za wanadamu na katika mpangilio ulio nzuri Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Ameyataja yote kwa pamoja: Kuhusu haki za Allah aya hii inaeleza kwamba Mwenyezi Mungu atiiwe kwa *adl* (kufanya haki / sawa na uhalisia/uadilifu) kwa sababu ametuumba, anatulea na anaendelea kufanya hivyo kwa kudumu. Ni haki yake kwamba nawe pia umuabudu. Na iwapo una uelewa zaidi basi usimwabudu tu kwa vile ni haki yake kuabudiwa lakini fanya kama *ihsan* (fanya kama njia ya kutenda wema/kulipa hisani) kwani fadhili na rehema za Allah hazina mipaka. Bila shaka hatua ya Ihsan (kulipa wema) iwapo itazingatiwa ni ya juu zaidi kuliko *adl*. Kujali kwa kudumu maana ya Ihsan kunapelekea kuziona rehama za Mwenyezi Mungu zikiwa bayana hivyo maana ya ihsan pia ni kumwabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba unamuona.

Kwa hakika watu wanaomwabudu Mwenyezi Mungu wako wa aina tatu. Ya kwanza ni wale ambao wanaabudu bila kuzingatia sifa za Mwenyezi Mungu ipasavyo kwa vile kwao Mungu haonekani wakati mambo ya kidunia yanaonekana. (Yaani wanaabudu kwa mtazamo wa kidunia/mtazamo wa juu juu tu). Jazba ile izalikayo kwa kukumbuka ukuu wa Mwenyezi Mungu haizaliki ndani mwao, na mapenzi yale yazukayo kwa kufikiria ukuu na hisani ya Mwenyezi Mungu hayaibuki ndani yao. Wanamkubali Mwenyezi Mungu kuwa ni muumbaji kwa mdomo tu bila ya kutafakari kwa makini juu ya sifa na ukarimu wa Mwenyezi Mungu, ambapo ni kwa kuzitafakari hizo tu ndipo hupelekea kuziona karama za Mwenyezi Mungu mbele ya macho. Mwako wa ladha za kidunia ndani yao hauwaruhusu kuona uwepo ulio wazi wa Muumbaji. Hawana uoni utoshao kumwona Mtowaji wa kweli. Uelewa wao wa Mwenyezi Mungu umechanganyika na mtazamo wa kidunia na kwa sababu ya hilo hawawezi hasa kupata uelewa wa msaada wa Mwenyezi Mungu. Hawana habari ya vipi hasa mtu anatakiwa awe anapomkumbuka hisani za Mwenyezi Mungu, hali ambayo ndiyo inayopelekea mtu kuona ukarimu na hisani ya Mwenyezi Mungu mbele ya macho yake. Uelewa wao na elimu yao juu ya Mwenyezi Mungu imefifia. Sababu ya hili ni kuwa wanategemea zaidi juhudi zao na njia zingine za kidunia na sababu nyingine ni kwamba wanakubali kama dhana tu sifa za Mwenyezi Mungu za uumbaji na kuruzuku. Kwa vile Mwenyezi Mungu hamshurutishi mtu zaidi ya uwezo wake basi kubwa analolitaka Mwenyezi Mungu kwa watu daraja hili ni hiki tu kwamba wawe na shukurani kwa ukarimu wake na maana ya: *'Hakika Mwenyezi Mungu Anaamuru uadilifu, …'* maana ya adl hapa itakuwa ni kufanya mambo kwa usawa yaani kumwabudu Mwenyezi Mungu kama haki yake.

Lakini mtu anaweza kupata hatua ya juu zaidi ya kumtambua na kumwelewa Mwenyezi Mungu, ambapo kama vile ilivyoelezwa hapo kabla, anakuwa juu zaidi ya mtazamo wa kijuu juu tu bali anafikia kuuona ukarimu wa Mwenyezi Mungu na rehema zake, na anajivua kwenye kiza cha kujali tu sababu na matokeo yake.

Sababu kama vile mazao yangu yalimea vizuri kwa sababu niliyamwagilia maji, au nilifanikiwa kwa sababu ya juhudi yangu niliyofanya au jambo langu hili na lile lilifanikiwa kwa sabbau ya msaada wa Zaid au niliokoka na maangamizi kwa sababu ya hisani ya Bakri, sababu hizo zinakuwa mbele yake ni vitu vidogo bali ni uongo.

Mtu anaona dhati Moja tu, nguvu Moja tu, Mruzuku/ Msaidizi Mmoja tu na Mkono Mmoja tu. Na ni baada ya hapo mtu anapoziona hisani za Mwenyezi Mungu kwa uwazi kabisa na bila ya mchanganyiko wa kutegemea sababu na athari zake. Dhihirisho hili linakuwa ni wazi na bayana kabisa kiasi hiki kwamba uwepo wa Mwenyezi Mungu hauwi ni dhana tena wakati anapoabudu bali Anakuwa ni dhati iliyo bayana kabisa mbele yake. Qurani Tukufu imeiita hatua hiyo ya kuabudu kuwa ni Ihsan na Mtume s.a.w. ameeleza maana hiyo hiyo ya Ihsan katika Hadithi ya Sahih Bukhari na Muslim.

Hatua inayofuata ni *'… kutoa kama kuwapa ndugu …'* maana yake ni kwamba wakati mtu anatumainia rehema za Mungu zaidi ya njia na sababu zake na anamwabudu Mungu kwa kumuelewa kwamba yupo na kwamba ndiye Mtoaji na Mpaji, hali hiyo na uelewa huo mwisho wake huzalisha mapenzi binafsi ya Mungu ndani yake. Tumaini la juu zaidi na la kudumu kwa Mwenyezi Mungu huzalisha athari ndani ya moyo ya kuwa mtu mwenye shukurani na moyo wake hujazwa mapenzi ya Mungu ambapo baraka zake hubakisha athari kwa mtu huyo.

Katika hali hiyo hamuabudu Mwenyezi Mungu kwa sababu ya hisia ya Ihsani, badala yake mapenzi binafsi ya Mungu huzuka ndani ya moyo wake mithili ya mtoto alivyo na mapenzi binafsi kwa mama yake. Hapo sio kwamba anamuona Mungu wakati wa kuabudu tu bali anajipatia ladha muda wowote kama vile mtu anayenyenyekea. Hili ndilo daraja ambalo Mwenyezi Mungu ameliita .. kutoa kama kuwapa ndugu wa karibu…' na amelitaja hili katika aya aliyosema: (2:201).

Na mwishapo kuzitimiza ibada zenu (za Haji), basi Mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama mnavyowakumbuka baba zenu au kumbukeni zaidi;

Kwa ufupi haya ndio maelezo ya aya hii: Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anaamuru uadilifu, na hisani, na kuwapa (watu kama uwapavyo) ndugu; na Anakataza upujufu, na uovu, na uasi. Anawanasihini ili mpate kufahamu. (16:91) …

Ndani yake Mwenyezi Mungu amezitaja hatua zote tatu za uelewa ambao mwanadamu anaweza kuupata juu ya Mungu na ameiita hatua ya tatu kuwa ni daraja la mapenzi binafsi. Hili ni daraja ambalo sababu zote za ubinafsi zinafutika na moyo unajazwa mapenzi mithili ya chupa ya uturi iliyotengenezwa kwa glasi ijazwayo manukato. Ni katika hatua hii tu ndipo aya

Endelea uk. 4

Jitahidini kupata Mapenzi ya Mungu

Kutoka uk. 3

hii inazungumza:
Na yuko miongoni mwa watu auzaye nafsi yake kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa watumishi.' (2:208)

Na pia inasemwa: Naam, ye yote anayejitupa kwa Mwenyezi Mungu, naye ni mtenda wema, basi yeye atapata malipo yake kwa Mola wake, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.… 2:113).

Yaani Mwenyezi Mungu na mapenzi ya Mungu vinakuwa ndio lengo lao na tarajio lao kuu na fadhili za Mungu zinakuwa ndio malipo yao. Mwenyezi Mungu anasema katika mahala pengine …
Na huwalisha chakula maskini na yatima na mfungwa kwa mapenzi Yake. (Husema): Tunawalisheni kwa ajili ya radhi ya Mwenyezi Mungu tu, hatutaki kwenu malipo wala shukurani. (76:9-10).
Ni jambo la kuzingatia kwamba aya hizi zote zinadhihirisha kuwa Qurani Tukufu imeielezea kuwa ni daraja bora kabisa kumwabudu Mwenyezi Mungu na kufanya matendo mema iwapo moyo unatafuta kwa ikhlasi mapenzi na radhi za Mwenyezi Mungu.
Ingawaje swali linalozuka ni hili kwamba, je Biblia inayo mafundisho mazuri kama haya yaliyoelezwa ndani ya Qurani tukufu? Tunamhakikishia kila mtu kwamba Biblia haijalieleza jambo hili kwa undani kama huu. Mwenyezi Mungu Aliyetukuka ameiita dini hii kuwa ni dini ya Islam kwa lengo hili kwamba mwanadamu amuabudu Mungu kutokana na sifa zake nzuri alizonazo kwa sababu Islam maana yake pia ni kuacha matamanio yote binafsi na kujinyenyekeza kwenye matakwa ya Mwenyezi Mungu. Hakuna dini nyingine duniani zaidi ya Islam iliyo na malengo haya. Bila shaka Mwenyezi Mungu kwa kuonesha ishara yake ya rehema amewaahidi waaminio wa aina zote fadhili zake, Ingawaje waaminio wanaokusudia kufikia daraja la juu wamefundishwa wamwabudu Mwenyezi Mungu kwa Upendo kwake. (Nur ul Haq, Jal. II, uk. 436- 441, Ruhani Khaza'in Vol. 9).

Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameandika yafuatayo kuhusiana na alama ya mapenzi ya kweli:
"Upendo ni kitu cha ajabu. Moto wake unakula moto wa dhambi na kuzima moto wa ukosefu wa utii. Hapawezi kuwapo swala la adhabu mahala penye upendo kamili na wa kweli. Mojawapo ya dalili za mapenzi ya kweli ni hii kwamba mpendaji anahofia hata wazo la kutengana na yule ampendaye. Anajiona ameshaangamia hata kwa kosa lake dogo sana, na anaona kumuudhi mpenziwe ni kama sumu yenye kuua.
Pia daima mawazo yake yanagubikwa na tamanio la kukutana na mpenzi wake, na kutokuwapo kwake na utengano nae huuondoa hata uhai wake. Hii ndio maana sio tu huyaona ni dhambi matendo ambayo huonwa ni dhambi na watu wa kawaida kama; kuua, kuzini, kuiba na kutoa ushahidi wa uongo, bali huona ni dhambi kubwa sana mkao wowote unaoelekea kuwa mbali hata kidogo tu na Mungu, kukijali kitu kingine chochote ambacho si Yeye Mungu.

Kwa hivyo wakati wote huomba ghofira na kufanya Istighfar kwa mpendwa wake wa milele. Kwa kuwa hawezi kuhimili utengano nae wakati wowote, kuzembea kokote atakakokufanya kwa sababu ya udhaifu wake wa kibinadamu kunaonekana kwake kama mlima wa dhambi.

Hii ndio sababu wale waliomo katika mahusiano matakatifu na ya kweli na Mungu, daima huwamo katika kufanya Istighfar. Mpendaji wa kweli ni mwenye wasiwasi isije mpendwa akaudhika nae, na moyo wake umejaa kiu cha kutaka kumpendeza kikamilifu, na hatosheki hata pale Mungu Mwenyewe anapomuarifu kwamba ameridhika nae. Kama ambavyo mlevi hatosheki na hunywa mara kwa mara na kila wakati anaomba zaidi, halkadhalika pale chemchem ya mapenzi ya Mungu inapotiririka katika moyo wa mtu, kwa kawaida hutaka kupata pendo lake zaidi kadiri inavyowezekana. Hivyo mapenzi zaidi hupelekea kwenye *Istighfar* kubwa zaidi. Hii ndio sababu wale walio wakamilifu katika mapenzi yao kwa Mungu daima wamo katika kuomba msamaha wa Mungu na dalili ya uhakika kabisa ya mtu asiye na dhambi ni hii kwamba mtu huyo hujishughulisha na Istighfar zaidi kuliko watu wengine. Maana ya kweli ya Istighfar ni kuomba kwa Mungu kwamba aondoshe uwezekano wowote wa kuvuka mipaka au ukosefu ambao mtu anaweza kuutenda kwa sababu ya udhaifu wa umbo la kibinadamu, na kwamba Afunike makosa yake na asiyaache kubainika.

Maana ya Istighfar vile vile hupanuka mpaka kwa watu wa kawaida na kwao wao humaanisha kuomba Mungu kwamba amlinde muombaji na matokeo mabaya na sumu ya kupita kwake kiasi na ukosefu wake, hapa duniani na akhera.

Kwa hiyo chanzo cha kweli cha wokovu ni kumpenda Mungu mapenzi ya kweli ambako huvutia pendo la Mungu kupitia unyenyekevu, maombi na Isitighfar ya mtu. Pale mtu anapoyafikisha mapenzi yake katika ukamilifu na moto wa mapenzi ukaunguza tamaa zake mbaya hapo mara moja mwako wa pendo alilonalo Mungu kwa ajili ya mtumishi wake huanguka kwenye moyo wa mtu huyo na humsafisha na uchafu wa maisha duni. Ndipo hupata sura ya utukufu wa Mungu, ambaye ni Hayyu na Qayyuum na hupakazwa sifa zote za Mungu kwa maana ya kuakisi (zill). Ndipo anachukua muonekano wa utukufu wa Mungu, na yote yaliyofichika katika hazina ya Mungu yanabainishwa kwa ulimwengu kupitia yeye, kwani Mungu Aliyeiumba dunia hii sio bahili, na rehema zake ni za milele na dawamu na majina yake na sifa Zake hazijawahi kukoma (*Chashma e Masihi, Fountain of Christianity*, uk. 57-59).

Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliandika juu ya ondoleo la dhambi: "Dhambi ni sumu ambayo huzaliwa pale mwanadamu asipomwabudu Mungu, asipompenda kwa huba na asipomkumbuka kwa mapenzi. Mtu ambaye moyo wake unatengana na pendo la Mungu ni kama mti ambao baada ya kung'olewa kutoka ardhini, na hivyo kushindwa kunyonya maji yoyote, unanyauka kila uchao na sio muda mrefu unapoteza haiba yote. Dhambi humparaganya mtu kama ukame unavyoua mmea. Sheria ya Mungu imetoa dawa tatu kwa ugonjwa huu. Ya kwanza upendo, ya pili Istighfar yaani kutamani kukiweka wazi kitu fulani. Kwa kadiri mizizi ya mti inavyobakia imefunikwa na udongo unao kila nafasi ya kubakia kijani, Ya tatu, kutubu yaani kugeukia kwa Mungu kwa unyenyekevu wote kunyonya maji ya uhai, kupata ukaribu Nae na ili kuachiliwa na kamato la kiza cha dhambi kwa njia ya matendo mema. Toba ya mdomo mtupu haitoshi. Toba ya kweli lazima iambatane na matendo mema ambayo humleta mtu karibu na Mungu. Sala pia ni aina ya toba kwa sababu kwayo twatafuta ukaribu na Mungu.

Hii ndio sababu pale Mungu alipopulizia uhai kwa mtu aliliita pulizo hilo ni Roho kwa kuwa furaha yake ya kweli imo katika kumtambua na kumpenda Mungu na kujitupa kwake. Ameiita pia nafsi kwa kuwa inatafuta maungano na Mungu. Yule ambaye anampenda Mungu ni sawa na mti ambao mizizi yake imejishika sawasawa ardhini. Hii ndio pepo ya juu kabisa ya mtu. Kama vile mti unavyonyonya na kujitwalia maji kutoka ardhini, na kuondosha vitu vyenye madhara kupitia ardhi, pale moyo wa mtu unapolishwa kwa maji ya mpenzi ya Mungu, inaweza kirahisi kuondosha athari zote zenye sumu. Baada ya kujizamisha kwa Mungu inaendelea kupata lishe safi na salama ambayo huiwezesha kukua na kuchanua na kutoa matunda. Lakini wale ambao hawana mizizi yao kwa Mungu hawawezi kunyonya maji haya yalishayo. Huendelea kunyauka kila muda uendao na majani yao yote huanguka yakibakisha matawi matupu yasiyopendeza. Kwa kuwa ukame wa dhambi hutokana na utengano, dawa ya dhahiri ni kujenga mahusiano madhubuti na Mungu, kama ambavyo sheria ya kimaumbile yenyewe inavyoshuhudia. Akikusudia hili Mungu Mwenye Enzi Anasema: ..... 89:28-31).

Kwa hiyo pendo la kweli na la dhati kwa Mungu, ndio dawa pekee ya kuondosha dhambi. Matendo ya ucha Mungu yatokanayo na mapenzi haya husaidia kuzima moto wa dhambi kwa sababu pale mtu anapofanya matendo mema kwa ajili ya Mungu hapo anathibitisha mapenzi yake Kwake. Hatua ya kwanza ya upendo, ambayo yaweza kubainishwa na mti ambao umepandwa ardhini, ni kuwa na imani kiasi hiki juu ya Mungu kwamba mtu humtumainia Mungu zaidi kuliko kitu kingine chochote, hata zaidi ya maisha yake. Hatua ya pili ambayo yaweza kulinganishwa na mti ambao umeotesha mizizi imara ardhini, ni Istighfar, ambapo mtu anakuwa anaogopa utengano na Mungu ambao utamuacha kweupe na mapungufu yake yakionekana.

Hatua ya tatu, ambayo inafanana na mti ambao mizizi yake imezama mpaka karibu na kuyafikia maji na kuyanyonya kama mtoto ni toba. Falsafa ya dhambi ni kwamba yatokana na mtu kujitenga na Mungu na hivyo yaweza tu kuepukwa kwa kujenga mahusiano Naye. Ni wajinga hasa wale wanaodai kwamba dhabihu ya mtu mwingine ndio ondoleo la dhambi zao. (Four Questions By A Christian And Their Answers', pp. 2-5).

Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliandika zaidi: katika Quran Tukufu Mungu ametupatia mafundisho kamilifu, ambayo yakifuatwa, yanatuwezesha kumuona katika maisha haya haya. Amesema: … Sema: Bila shaka mimi ni binadamu kama ninyi; inafunuliwa kwangu ya kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Basi anayetumaini kukutana na Mola wake, na afanye vitendo vizuri wala asimshirikishe ye yote katika ibada ya Mola wake. (18:111).

Yaani, yeyote anayetaka kumuona Mungu – Muumbaji wa kweli – katika maisha haya, aenende kwa taqwa, matendo yake yasiwe na hila, fahari, majivuno, maringo na yasiwe mabovu, au mapungufu au kinyume na mapenzi aliyonayo kwa Mungu, na badala yake yawe yamejawa na ukweli wa moyo na uaminifu. Anapaswa pia kujiepusha na shirki na asiliabudu jua, au mwezi, au nyota, au hewa, au moto, au maji, wala kingine chochote. Anapaswa pia asiweke tumaini lake kwenye njia za kimwili kama vile hizo ni washirika wa Mungu; wala sitegemee nguvu zake mwenyewe. Kwa maana kufanya hivyo nako ni sawa na shirki. Baada ya kufanya kila analolielewa, anatakiwa aone hayo yote sio chochote na asijivunie elimu yake au juhudi zake, na anatakiwa ajione hajui kitu na hana uwezo wowote. Roho yake yapaswa siku zote ione imejitupa katika kizingiti cha Mwenye Enzi, ikitafuta rehema yake kwa sala na maombi. Kwa hiyo mnatakiwa muwe kama mtu mlemavu mwenye kiu ambaye anaona chemchem ya maji safi na anajaribu kuyafikia akichechemea huku akijikwaa na kuanguka, na pale hatimae anapoweka mdomo wake hapo majini haachii mpaka kiu yake imeisha kabisa. (*Lecture Lahore,* uk. 10-11).

Masihi Aliyeahidiwa a.s. pia alisema: Ikiwa utagundua ya kwamba unao uwezo wa kupenda kuwa mtumishi mkweli na thabiti, ambaye huvumilia njaa na kiu pale anapotengenishwa na mpenziwe na hajali tena chakula au kinywaji au mwili wake, basi jiweke kwenye mapenzi na Mungu, kwa namna hii kwamba nafsi yako mwenyewe ipotee mahala fulani katika njia hiyo. Mtu ana bahati njema sana ikiwa anafariki akiwako katika hali hii. Tunahusika na mapenzi binafsi na sio funuo na maono. Mnywaji hunywa kikombe baada ya kikombe cha pombe na hupata burudiko. Hivyo hivyo mwenye kikombe cha mapenzi kwa Mungu, kama vile mlevi asivyotosheka, nanyi pia kamwe msitosheke. Mtu asirudi nyuma kamwe mpaka ufikie wakati ambao amefikia hatua ile katika kupenda kwake ambayo anaweza kuitwa mpendaji mwenye shauku kali. Anatakiwa kutembea mbele na juu zaidi bila hata kidogo kukiachia kikombe. Jiwekeni kwenye hangaiko na taabiko kwa ajili ya hicho. Kama hujafikia hatua hii basi huna maana yoyote. Mapenzi kwa Mungu yapaswa kuwa hivi kwamba kingine chochote hakiwi na thamani mbele yake. Msianguke kwenye tamaa yoyote na msihofie chochote kitiacho hofu. (*Malfuzat, Vol. 3, p. 134, new edition*)
Masihi Aliyeahidiwa a.s alisema 'Pale mtu anapokuwa na amani na Mungu Mwenyezi kikamilifu na hana malalamiko yoyote

Endelea uk. 5

Jitahidini kupata Mapenzi ya Mungu

Kutoka uk. 4

ni wakati huo ndipo anajenga mapenzi ya kumpenda Mungu. Bila ya kujenga mapenzi kwa Mungu imani imo kwenye hatari kubwa na mapenzi ya Mungu yanapojengeka mtu anapata kusalimika kutoka kwenye mashambulio ya shetani. Mpaka mapenzi haya yanapokuwa yamejengeka mtu anabakia katika hali ya *nafse Ammarah* (nafsi inayoita kwenye maovu) na anakuwa amezingirwa nayo. Watu walio chini ya *nafse Ammarah* hupenda dunia hii na huona akhera ni mbali, wapo mahala pabaya sana. Na wale waliopo chini ya msukumo wa *Nafse Lawamah* (nafsi inayojilaumu) ni marafiki wa Mungu wakati fulani na wa shetani wakati mwingine. Hawabaki na hali moja kwa kuwa wanapigana na nafsi na katika mapambano hayo wakati mwingine wanashindwa. Hata hivyo, watu hawa wako mahali pazuri kwa sababu hutenda matendo mema na humuogopa Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, ni wale tu waliopo chini ya msukumo wa *Nafse Mutmainnah* (Nafsi yenye faraja) ndio washindi. Huziacha hatari zote na hofu zote nyuma na hufikia mahala pa amani na wapo katika malezi ya amani ambapo shetani hawezi kupafikia. (*Malfuzat, Jal. 3, uk. 508, new edition*).

Masihi Aliyeahidiwa a.s anasema: Mwaminio anayo rangi ya mpendaji anayependa kwa shauku kubwa na yu mkweli katika pendo lake la shauku. Hamu yake kwa mpenziwe ambaye ni Mungu, ni ya kujitoa kabisa kwa mapenzi na uamnifu na hujitupa kwa Mungu kwa unyeunyekevu, maombi na uthabiti. Hakuna faraja ya kidunia ambayo ni faraja kwake na roho yake hulelewa kwa mapenzi ya Mungu. Hakasirishwi kwamba mapenzi yake hayapati na hakatishwi tamaa anapoona kimya na anapokosa jibu kutoka kwake. Kwa hakika daima huwa anasonga mbele na juu zaidi na huonesha ulainifu zaidi na zaidi wa moyo. Ni muhimu kuwa nazo sifa hizi mbili kwamba mwaminio mwenye shauku awe amezama katika kumpenda Mungu na mapenzi yake ya shauku kubwa yawe ya kiwango cha juu.

Hamu ya kweli ya mapenzi na uthabiti wa maamuzi katika nia yake ya kupenda yapaswa kuwa yamezama ndani yake kiasi hiki kwamba hakuna tatizo litamtelezesha katika nyakati kuwapo na ukimya na kukosekana kujaliwa na mpenziwe. Anatakiwa awe na aina mbili za ulainifu. Moja ulainifu wa mapenzi kwa Mungu na mwingine ambao huzalika moyoni kutokana na taabu za watu wengine na hangaiko hutokea kwa ajili ya faraja yao na mtu hukosa utulivu ili kuwasaidia.

Uaminifu wa moyo na ulainifu kwa mapenzi kwa Mungu pamoja na uthabiti wa maamuzi humtenga mtu na ubinaadamu humweka kwenye mpaka mapenzi yake kwa Mungu yanapofikia hatua ambapo anakuwa si mhitaji wa chochote ila Allah. Ni vigumu kuishinda hatari hii na ni vigumu pia kuingia katika ulingo wa radhi Yake isipokuwa kwa kukata mahusiano yote ila yale ya Allah pekee. Mtu anahitaji kuwa na ulainifu kwa viumbe wa Mungu kama mapenzi ya dhati ya mama anayemjali kwa mapenzi, mtoto wake mchanga. (*Malfuzat, Vol.4, p.32, newedition*).

Masihi Aliyeahidiwa a.s alisema: Uhusiano imara na mapenzi ya dhati na Mungu Mwenye Enzi huzalika pale mtu anapotambua Mungu Alivyo. Watu wamejawa na dhana. Wengi wamekuwa wapagani wazi wazi wakati wengine ambao hawakuwa wapagani lakini wanashawishiwa nao kwa sababu wamekuwa hawajali mambo ya imani. Suluhisho kwao ni kuendelea kuomba kwa Mungu ili kwamba uelewa wao juu ya Mungu upate kuboreka. Wakae pamoja na wakweli ili waweze kushuhudia ishara mpya za nguvu na adhama ya Allah mwenye Enzi. Hapo atawaongezea uelewa wao kama atakavyopenda na kwa namna atakayopenda na kuwapa uono…

Ni kweli kabisa kwamba kadiri imani iwavyo kubwa juu ya kuwapo na utukufu wa Allah mwenye Enzi ndivyo kadiri mtu anavyoogopa na anakuwa na hofu juu ya Allah Mwenye Enzi. Vinginevyo mtu anakuwa hajali kuhusu dhambi katika nyakati za kughafilika.

Mapenzi ya Allah mwenye Enzi na hofu na kuogopa juu ya utukufu wake ndio hisia mbili zinazounguza madhambi. Ni jambo la kawaida kwamba mtu hukiepuka kile anachokiogopa. Kwa mfano ikiwa anajua kwamba mahali fulani pana nyoka hatokwenda hapo. Vile vile ikiwa atajua kwamba sumu ya dhambi itamwangamiza na anaogopa utukufu wa Mungu mwenye enzi na anajua kwamba Mungu hapendi dhambi na hutoa adhabu kali kwa ajili yake, hatajiachilia katika kutenda dhambi. Anatembea ardhini kama vile hana uhai mwilini mwake. Roho yake daima inakuwa kwa Mungu (*Malfuzat, Vol. 4 pg 404, new edition*).

Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliandika: Pale mtu anapoachana na nafsi yake yote kwa kuanguka katika mapenzi kwa Mungu Mwenye Enzi, kile kile kifo kwa mapenzi humpatia maisha mapya. Hamuwezi kuelewa kwamba mapenzi pia ni kama moto na dhambi pia ni kama moto? Moto wa mapenzi kwa Mungu huzima moto wa dhambi, na huu ndio msingi wa wokovu. (*Qadian Key Arya Aur Hum pg*. 448, *Ruhain* Vol. 20).

Masihi Aliyeahidiwa a.s aliandika. Mungu humwokoa mtu ambaye ni mcha Mungu kweli kutoka kwenye majanga sio kwa namna ya kawaida bali kama ishara. Kila mtu aliye tapeli au mjinga hudai kuwa mcha Mungu, lakini pekee yu mcha Mungu yule ambaye anathibitishwa na ishara ya Mungu. Kila mtu aweza kusema anampenda Mungu, lakini pekee yu mpenda Mungu yule ambaye pendo lake limethibitishwa na ushahidi wa Kimbingu. Na kila mtu husema dini yangu ni ya kweli, lakini pekee yu mwenye dini ya kweli yule ambaye anapewa nuru katika dunia hii hii. Na kila mmoja husema nitapata wokovu, lakini pekee yu mkweli katika kusema hilo ambaye huiona mianga ya wokovu katika maisha haya haya. Kwa hivi jitahidini muwe wapendwa wa Mungu ili muokolewe na kila janga (*Kishti Nuh. P 82, Ruhani Khazain* Vol. 19).

Ni mwenye bahati mbaya kiasi gani mtu yule ambaye bado hajui kwamba yupo Mungu mwenye nguvu juu ya kila kitu. Pepo yetu imo katika Mungu wetu. Furaha yetu kubwa kabisa iko kwa Mungu wetu kwa kuwa tumemouna na tumeukuta kila aina ya uzuri ndani yake. Utajiri huu yafaa kuununua hata mtu akibidika kutoa maisha yake ili kuupata. Rubi hii inafaa kuinunua hata mtu akibidika kuipoteza nafsi yake ili kuipata. Enyi wenye uhitaji kimbilieni kwenye chemchem hii na itawatosheni. Ni chem chem ya uhai itakayowaokoeni. Nifanye nini, ni kwa namna gani nitilie nyoyoni habari hizi njema, na kwa kupiga ngoma gani ninadi tangazo kwamba huyu ndiye Mola wetu, ili kwamba watu waweze kusikia? Niweke dawa gani katika masikio ya watu ili waweze kusikia?

Kama ninyi mtakuwa wa Mungu, fahumuni kwa yakini kuwa Mwenyezi Mungu pia atakuwa wa kwenu. Mkiwa mmelala, Mwenyezi Mungu atawalindeni. Mkiwa mmeghafilika juu ya adui zenu Mwenyezi Mungu, Atawaangalieni na atavunja hila zao. Mpaka sasa hamjajua uwezo wa Mungu wenu, lau kama ninyi mngalijua haya isingetokea siku yoyote ninyi kuhuzunikia dunia yenu. Mtu mwenye hazina akipoteza pesa moja analia au anapiga kelele au anajiangamiza? Basi lau kama mngalijua habari za hazina hii, ya kwamba Mungu wenu anaweza kuwasaidieni katika kila wakati wa haja msingalihangaika kupenda dunia. Mwenyezi Mungu ni hazina ipendwayo, iheshimuni. Yeye ndiye msaidizi wenu katika kila mahali. Ninyi si kitu, wala vitu vyenu wala hila zenu si chochote pasipokuwa Yeye.

Msifuate mataifa yaliyoangukia na kutawakali juu ya vitu na hila zao, Wao wamekula udongo wa vitu vya dunia kama nyoka anavyokula udongo. Na kama mbwa na mbesi wanavyokula nyamafu (mzoga), hivi ndivyo wao wameuma nyamafu. wamekuwa mbali sana na Mwenyezi Mungu. Wamewaabudu watu na wamekula nguruwe na wametumia pombe kama maji na wamehilikishwa kwa sababu ya kuangukia kwao kwenye vitu na kuacha kuomba nguvu kwa Mungu. Na roho ya mbinguni imeruka kutoka kwao kama njiwa anavyoruka kutoka katika kiota. Katika mioyo yao mna ukoma wa kupenda dunia uliovikata viungo vya ndani yao vyote. Basi jihadharini na ugonjwa huu! (*Kishti Nuh pp 21 – 22, Ruhani Khazain Vol*. 19).

Mwapaswa kufanya juhudi kubwa ya kumtambua Mungu ambamo katika kumjua ndimo uliomo uokovu wa kweli na kufuzu kweli. Mungu yule pia hujionesha kwa wale wanaomtafuta kwa uaminifu wa moyo na mapenzi. Hujionesha kwa yule ambaye amekuwa wa kwake. Nyoyo takatifu ndiyo nyumba yake na ndimi ambazo hazisemi uongo na ubabaishaji ndio huwakilisha funuao zake. Na kila mtu ambaye amezama kabisa kunyenyekea kwenye radhi ya Mungu, humjia kwa onesho la nguvu zake za kimiujiza. (*Kashful Ghita, p 188, Rohani Khazain, Vol*. 14).

Mwenyezi Mungu na atuwezeshe kufikia viwango ambavyo Masihi Aliyeahidiwa a.s alivitazamia kwetu na atuwezeshe kugeukia Kwake kwa uaminifu wa moyo na kufikia pendo lake na sote tuingizwe katika bustani ya Radhi Yake. Amin.

Ahmadiyya yatoa Maji na Umeme Afrika

Na Pazi Mazongera

Kiongozi wa jumuiya ya Waislam Ahmadiyya duniani, Hazrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. ametoa wito kwa wahandisi wa Jumuiya hiyo (IAAAE) waendelee kuitumikia Afrika bilhususi juu ya upatikanaji wa maji tena maji yaliyo salama.

Akizungumza kwenye kongamano la wahandisi wa Kiahmadiyya lililofanyika jijini London, Kiongozi huyo wa Waislam duniani alisema, Ni kweli katika Afrika watu wengi hawapati maji yaliyo salama, hivyo Kuwabidi kutembea maili nyingi kuyafuata maji.

Akizungumzia uzoefu wake wa kuishi na kufanya kazi barani Afrika, Kiongozi huyo alisema, Ni katika kuishi na kufanya kazi Afrika ndipo alipotambua kuwa tatizo sio tu maji bali ni maji safi na salama.

Aliendelea kwa kusema "Nimeona kwa macho yangu watoto wadogo wakitembea mwendo wa maili mbili hata tatu wakitafuta maji". Alisema ni jambo la kusikitisha kuwa hali hii bado inaendelea.

Alisema "Mimi binafsi ilinibidi baadhi ya wakati nisafiri zaidi ya maili kumi kufuata maji kwa matumizi yangu ambapo nilijaza kwenye vyombo na kuyasafirisha kwa gari ndogo. Kama nilivosema ni pale tu ambapo mtu anatumia juhudi kupata maji ndipo unapogundua thamani yake. Alisema Khalifa Mtukufu katika nasaha zake.

Aidha,Hazrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. alizungumzia jinsi wahandisi hao walivyotekeleza maelekezo yake ya kuanzisha vijiji vya mfano katika maeneo yasiyofikika katika Afrika. Hii itajumuisha kuwekwa kwa taa za mitaani, nyumba bora, vituo vya kijamii, mitaa pamoja na upatikanaji wa maji safi ya kunywa kirahisi.

Akizungumzia juu ya mpango huu Hazrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. alisema " watu wale ambao waliishi katika ardhi ambayo hapo kabla haikuwa na huduma yeyote na katikati ya msitu wanabaki wakishangaa" aliendelea kwa kusema " hawajawahi kufikiri kuwa nyumba zao zingekuwa na umeme au maji au kuwa mitaa yao ingetengenezwa. Kwa watu hawa huduma kama hii hawawezi kuamini na furaha yao ni ya hakika." Alisema.

Khalifa Mtukufu alisema kuwa katika vile vijiji ambavyo Waahmadiyya wanaishi wahandisi hawa wameweka huduma ya MTA. Katika njia

Endelea uk. 6

Bustani ya Washairi

ONDOKA

1 Ondoka kwangu ondoka, adui mwenye kibyongo
Ondoka tena ondoka, ni hafifu lako jengo
Ondoka sije tapika, ondoka ewe uongo
Ondoka!

2 Uongo una shabuka, mithili ya kikaango
Huileta patashika, watu hufunga milango
Kila unapotamka, zumo huyo ni muongo
Ondoka!

3 Kusema kweli daima, ni dhamira na kiwango
Kiwango cha taadhima, nisipate tena pengo
Nisadi Mola Karima, niache hiki kitengo
Ondoka!

Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)
Kiwalani Dar es Salaam

MLAZE PEMA PEPONI

1. Nakuomba Rahmani, wa rehema na karimu
Wepesi wa kifuani, mkono shika kalamu
Nami niweze kughani, unipe na ufahamu
Mhariri asilani, umpe Baraka zako

2. Alipeme kwa makini, baba yangu Khamsin
Shairi liwe la shani, alipime kwa mizani
Kama lina walakini, asitoe gazetini
Mungu unipe Baraka, nami niweze kughani

3. Moyo una msituko, kwa nguzo ilodondoka
Tumepata fadhaiko, kwa baba kutuondoka
Kwa kweli ni tikisiko, huu ulio tufika
Rabi mwenye utukufu, mlaze pema peponi

4. Hamidu bini Muhimu, kusini ni mzaliwa
Siku yake ilitimu, mauti kwake kutuwa
Dunia si ya kudumu, sisi sote ni mauwa
Rabi mwenye utukufu, mlaze pema peponi

5. Msamehe baba yetu, rohoye iweke pema

Tunakuomba Mola wetu, mwenye sifa ya huruma
Nyoyo ziondowe kutu, nasi tulobaki nyuma
Rabi mwenye utukufu, mlaze pema peponi

6. Msiba huu mzito, leo tunajililia
Yamekithiri majuto, kwa ndani twaungulia
Kweli dunia mpito, baba tunakulilia
Rabi mwenye utukufu, mlaze pema peponi

7. Kaditamati watama, kituoni nimefika
Rabi twaomba salama, mjao akishafika
Apate yaliyo mema, peponi kupumzika
Rabi mwenye utukufu, mlaze pema peponi

Bi. Muhaimina Hamidu (Mmatumbi Asilia)
Duthumi – Morogoro, makazi mapya Mpanda

PANGA LIKISHIKA KUTU

1. Wanakwetu tafadhali, tafadhali wana kwetu
Msichezee makali, panga likishika kutu
Hiyo kubwa idhilali, ilowasibu wenzetu
Panga likishika kutu, usichezee makali

2. Japo limeng'ang'anaa, limekauka kwa kutu
Maizi hiyo hadaa, kushika usithubutu
Usende kuchuchumaa, makalio tufufutu
Panga likishika kutu, usichezee makali

3. Chini ya mpoopoo, palikuwapo na chatu
Alimeza majongoo, wawili au watatu
Nadhani hata kondoo, kawatia makulatu
Panga likishika kutu, usichezee makali

4. Alikuwepo jirani, jina aitwa nyamatu
Kalishika mkononi, panga chafu tena butu
Akampiga kichwani, kabakia macho pitu
Panga likishika kutu, usichezee makali

5. Ndugu zangu kwaherini, maswali nimeshafutu
Mwenye akili kichwani, hayatawaudhi katu
Ila wale afkani, wakichukia si kitu
Panga likishika kutu, usichezee makali

Sihiyana Swalehe Mandevu
(Mtenda mema)
Buguruni Malapa - Dar es Salaam.

SI HADAWE NA DUNIA

1. Ewe ulo na busara, fikiri bibi na bwana
Fikri lilo tohara, na lile lilo dhamana,
Pia fikiri izara, wewe nayo kukutana
Si hadawe na dunia, na dunia ina mwisho

2. Ujana ni jambo bora, ameupamba Rabana.
Tena umetia fora, ulitendalo hutuna
Basi usiwe mkora, akiba uweke sana
Si hadawe na dunia, na dunia ina mwisho

3. Kumbuka jambo dharuram jihimu kuweka sana.
Siyo pato kulipura, kwa usiku na mchana
Ukitoweka ujura, elewa umekubana
Si hadawe na dunia, na dunia ina mwisho

4. Hebu zituze fikira, ushike ninayonena
Akiba kwako sitara, ukiijaza shehena
Na pia huwa kafara, na shida isije tena
Si hadawe na dunia, na dunia ina mwisho

5. Ufanyapo biashara, ewe kijana kazana
Ujihimu kila mara, na akiba kushikana
Uzee ukidorora, uwe umetulizana
Si hadawe na dunia, na dunia ina mwisho

6. Kwa kweli si masiahara, mwanadamu hutatana
Kukosa kitu ni dhara, jina hotujulikana
Au uitwe fukara, uzee mja wa lana
Si hadawe na dunia, na dunia ina mwisho

7. Ujana hukuzingira, ukangiwa na fitina
Ukafikwa na majira, uzee ukawa jina
Basi na wako ujira, wakazi weak hazina
Si hadawe na dunia, na dunia ina mwisho

8. Kaditama natuwama, na kalamu kuachia
Na jina kujitangaza, mheshimiwa Magana
Mmeda tawi kung'ara, Masihi kumtangaza
Si hadawe na dunia, na dunia ina mwisho

Mwl. Ally S. Magana – Mmeda.

NIDHAMU YA JUMUIYA

1. Alinena Rasuli, kwa ajili ya motoni
Mdomo usotulia, nidhamu kutobaini
Waweza kutumbukia, mwisho wako hatiani
Nidhamu ya Jumuiya, sijasiri kubeua.

2. Nidhamu ya Jumuiya, si kama ya duniani
Wapo waloambulia, kutolewa nidhamuni
Hata kuwakumbukia, hawana yao thamani
Nidhamu ya Jumuiya, sijasiri kubeua.

3. Tunasoma Bukharia, cha mtawa mwenye shani
Rasuli ameusia, linenwalo mdomoni
Mwenyezi kasirikia, semi mbaya ya motoni
Nidhamu ya Jumuiya, sijasiri kubeua.

4. Hoja waweza letea, hujawekwa darasani
Mitaala fundishia, ndiyo iwe fikirani
Mimi takusaidia, kiburi usibaini
Nidhamu ya Jumuiya, sijasiri kubeua.

5. Mwenyezi sisitia, lichosikia tiini
Masroor Khalifia, kaeleza kwa makini
Machache kaandikia, kitabu chake someni
Nidhamu ya Jumuiya, sijasiri kubeua.

6. Shariti Baiatia, twendeni tudurusuni
Leo kimetufikia, kwa lugha ya kinyumbani
Shartile la kumia, kaeleza ya rohoni
Nidhamu ya Jumuiya, sijasiri kubeua.

7. Wengi wanopotea, kusoma hawathamini
Huridhia mazoea, liyoyakuta zamani
Hata walotangulia, yaliwaangusha chini
Nidhamu ya Jumuiya, sijasiri kubeua.

8. Na hata ukijifua, elimu kuibaini
Utawa wahitajia, Mwenyezi akuauni
Nina mengi ya kutoa, leo yakutosheeni
Nidhamu ya Jumuiya, sijasiri kubeua.

Twaha A. Nyange – Dar es Salaam.

Ahmadiyya yatoa Maji na Umeme Afrika

Kutoka uk. 5

hii, na kwa mara ya kwanza, wenyeji wameweza kumuona na kumsikia Khalifa wa zama. Aliendelea kwa kutoa mfano wa furaha ya Mzee Ahmadiyya toka Afrika kwa kuweza kumuona Khalifa kwa mara ya kwanza. Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. alisema " alipokuwa akiniangalia kupitia MTA machozi yalimtiririka Mzee Ahmadiyya toka Afrika. Alisema kwamba alikuwa akijiuliza kuwa ni lini ataweza kusikia maneno ya Khalifa moja kwa moja na leo Allah ametimiza maombi yake." Alisema kuwa Mzee huyo alikuwa akidhani kwamba angefariki bila ya kuweza kusikia sauti ya Khalifa wa zama na kitendo cha kusikia sauti hiyo kimemuacha katika hisia ya furaha ambayo hana maneno ya kweli ya kuelezea. Alimalizia Khalifa Mtukufu. Katika kuhitimisha nasaha zake kwa wahandisi hao, Khalifa Mtukufu alizungumzia juu ya faida na jukumu kubwa walilo nalo wahandisi hao kwa maelfu ya watu.

Hazrat Mirza Masroor Ahmad alisema " katika maeneo ya vijijini wahandisi hao si tu wameweza kutoa maji na kukata kiu kwa walio na shida hiyo hapo kabla, si tu wameweza kuwapatia maji ya kuoga na kuondoa uchafu katika miili yao, si yo tu kwamba wameweza kuweka mwanga kwenye majumba na mitaa iliyokuwa kizani. Lakini pia katika njia ya kiroho wamewaza kukata kiu ya kwa Wahmadiyya kuweza kumuoa na kumsikia Khalifa wa zama. Wameweka pia fursa na njia ya kujisafisha kiroho na kutakasa nafsi za watu kwa kuwapatia wenyeji huduma ya MTA na hivyo kuviangaza vijiji hivyo kwa mwanga wa kiroho, Alimalizia Khalifa Mtukufu nasaha zake kwenye kongamano hilo la Kimataifa la wahandisi waliohudhuria zaidi ya mia moja na kumi toka nchi za Ubelgiji, Uholanzi, Ujerumani, Uhispania, Uswizi na Uingereza.



Mzee Saeed Lone (kati kati) akiwa kwenye picha ya pamoja na wanajumuiya wa Zanzibar baada ya uchimbaji wa kisima kwenye eneo la Jumuiya.

Sheikh K. Amri Abedi Atunukiwa Nishani

Kutoka uk. 1

Gharib Bilali, Mh. Pinda n.k, hali iliyoashiria kuwa karibuni Mheshimiwa Raisi naye ataingia.

Hatimaye Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete aliingia ukumbini na watu wote wakasimama na wimbo wa Taifa kufuatia.

Watu wote waliketi baada ya Mheshimiwa Rais Kikwete kuketi. Mkurugenzi wa huduma za Ikulu, Bw. Julius R. Mogore alisimama na kumkaribisha Mheshimiwa Rais aanze shuhugli ya kutunuku nishani na Tuzo kwa wateuliwa.

Kulikuwa na nishani kadhaa na tuzo zilizokuwa zitolewe siku hiyo na mheshimiwa Rais. Nishani ya kumbukumbu ya miaka hamsini ya muungano (order), ilikuwa itolewe kwa waasisi wa muungano wa Tanzania pamoja na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano (aliye hai au marehemu), aliyeingia na kutoka madarakani kikatiba na kuendelea kuonyesha maadili mema na kuwa mfano wa kuigwa, ambaye katika kipindi cha uongozi wake, aliutetea, kuusimamia, kuuenzi, kuulinda, kuudumisha na kuuendeleza Muungano.

Nishani hii walikabidhiwa Waheshimiwa marehemu Julius K. Nyerere, iliyopokelewa na mjane wake Mh. Bi Maria Nyerere, Mh. Abeid Amani karume iliyopokelewa na mjane wake mama Karume, Mh. Ali Hassan Mwinyi, iliyopokelewa na mwakilishi wake na Mh. Benjamin William Mkapa aliyeipokea mwenyewe.

Halafu kulikuwa na nishani ya kumbukumbu ya miaka 50 ya Muungano daraja la kwanza iliyotunukiwa na Rais kwa waheshimiwa, Aboud Jumbe Mwinyi iliyopokelewa na mwakilishi wake, Marehemu Rashid Mfaume Kawawa iliyopokelewa na mwakilishi wake, John Samweli Malecela iliyopokelewa na mwakilishi wake, Cleopa David Msuya aliyeipokea mwenyewe, Joseph Sinde Warioba aliyeipokea mwenyewe, Omar Ali Juma iliyopokelewa na mwakilishi wake, Idrisa Abdul Wakil iliyopokelewa na mwakilishi wake, Salmin Amour Juma aliyeipokea mwenyewe na Amani Abeid Karume aliyeipokea mwenyewe.

Hawa walikuwa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Rais wa Zanzibar aliyeingia na kutoka madarakani kikatiba na kuendelea kuonyesha maadili mema na kuwa mfano wa kuigwa, ambao katika kipindi cha uongozi wao waliutetea, kuusimamia, kuuenzi,kuulinda,kuudumisha na kuuendeleza Muungano.

Kisha zikafuata nishani za kumbukumbu za miaka 50 ya Muungano, daraja la pili, kwa wale waliokuwa ndani ya Baraza la Mapinduzi (1964), Baraza la Mawaziri wa Tanganyika (1964) na viongozi wastaafu, walio hai au marehemu, ambao katika vipindi vyao vya uongozi, waliutetea, kuusimamia, kuuenzi,kuulinda,kuudumisha na kuuendeleza Muungano na waliendelea kuonesha maadili mema na kuwa mfano wa kuigwa hata bada ya utumishi wao.

Marehemu Sheikh Kaluta Amri Abedi alikuwa ni miongoni mwa watu hawa waliotunukiwa nishani hii iliyipokelewa na mwanawe Sheikh Bakri Abedi Kaluta, Mbashiri wa Jumuiya ya waislamu Waahamdiyya, anayekiongoza kitengo cha dawati la Kiswahili, Morogoro, Tanzania, aliyevalia koti jeupe la achken na kofia nyekundu ya tunga iliyofanana kwa kiasi fulani na ile aliyokuwa akiivaa marehemu Sheikh Kaluta Amri Abedi. Sheikh Bakri alipokuwa akiipokea tuzo alimsalimu Mheshimiwa Raisi kwa amkizi la Assalaamu Alaikum Warahmatullahi Wabarakatuh ambapo Mheshimiwa Raisi alijibu kwa furaha na bashasha iliyoandamana na tabasamu asilia; "Unaishi wapi?" Mheshimiwa Rais alimuuliza Sheikh Bakri, "Naishi Morogoro" lilikuwa jibu la Sheikh Bakri kwa Mheshimiwa Rais. "Ahaa unafanya nini huko?" Mheshimiwa Raisi aliuliza tena, na Sheikh Bakri hakufanya ajizi bali alimjibu: "Mimi ni miongoni mwa masheikh wa Ahmadiyya ninayeongoza dawati la Kiswahili lenye kutafsiri vitabu vya Jumuiya katika lugha ya Kiswahili." Mheshimiwa Raisi akaona shauku ya wapiga picha waliokuwa tayari wamezitegesha kamera zao kuchukua picha wakati sheikh Bakri akikabidhiwa tuzo hiyo kwa nioaba ya baba yake, marehemu Sheikh Amri Abedi Kaluta. "Haya bwana tazama kamera tupige picha", Bashasha ya mheshimiwa Raisi ilimvutia sana Sheikh Bakri na tabasamu la sheikh Bakri wakati wa kupiga picha lilitoa taswira halisi ya furaha iliyokuwa moyoni mwake, ingawa si rahisi kwa tabasamu hilo kulipiku tabasamu asilia la Mheshimiwa Raisi Kikwete.

Wengine waliotunukiwa nishani hii ni waheshimiwa Edward Moringe Sokoine, Salim Ahmed Salim, Fredrick Tulway Sumaye,, Brg. Gen. Ramadhani Haji Faki, Shamsi Vuai Nahodha, Thabit Kombo Jecha, Col Seif Bakari Omari, Mej. Gen. Abdallah Saidi Natepe, Brig. Gen. Yusuf Himidi Maftah, Hafidh Suleiman Almasi, Khamis Darwesh Mdingo, Pili Khamis Mpera, Saidi Idi Bavuai, Said Washoto Mnyuke, Hamid Ameir Ali, Mej. Gen. Khamis Hemed Nyuni, Mohamed Abdallah Ameir, Edington Herbat Kisasi, Hasnu Makame Mwita, Mohamed Juma Khamis, Mohamed Mfaume Omari, Muhsin bin Ali Juma, Daud Mahmud Jecha, Asanterabbi Zephania Nsilo swai, Paul Bomani, Habib Amir Jamal, Lawi Nangwanda Sijaona, Saidi Ali Maswanya, Solomon Nkya Eliufoo, Clement George Kahama, Job Malecela Lusinde, Dereck Noel Maclean Bryceson, Austin Kapera Shaba, Chief Adam Sapi Mkwawa, Ali Khamis Abdallah, Augustino Said, Augustino Stephen L. Ramadhan, Danstan Alfred Omari, Dickson Anitishe Nkembo, Makame Mzee Selemani, Suleiman Ali Mnoga, Mark Danhi Bomani na Idi Pandu Hassan.

Halafu zilizfuatia nishani za kumbukumbu za miaka 50 ya Muungano, daraja la tatu, zilizotolewa na Mheshimiwa Rais kwa waheshimiwa Zakhia Hamdan Meghji, Gen. Mrisho Sam Haggai Sarakikya, Gen. Abdallah Twalipo, Gen. David Bugozi Musuguri, Gen. Davis Adolf Mwamunyange, Elangwa Narundu Shaidi, Hamza Aziz Ali, Samwel Huma Pandugu, Ernest Jumbe Mangu, Obadiah Kingonyi Rungimbana, Ramadhani Kirungi Nyumba, John Casmir Minja.

Pia zilikuwepo nishani za kumbukumbu ya mikaa 50 ya muungano daraja la nne zilizokabidhiwa kwa waheshimiwa mama Maria Nyerere, Fatma Karume, Ali Mwinyikondo Mwinyigogo, Bwana Said Mabera wa Msondo Ngoma, Vicky Nsilo Swai, Hadija Abasi, Sifael Kunda Shuma, Hasamieli Elisach Mrema na Hassan Omar Mzee.

Nishani za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania daraja la pili zilikabidhiwa kwa Mabwana Buruda Anthony Canterussi na Rajan C. Kanabar.

Na tuzo maalum zilitolewa kwa mabwana Mark Green, Hayao Nakayama na Reginald Abraham Mengi.

Major D. J. Kobelo ndiye aliyekuwa akiita majina ya watunukiwa.

Hatimae picha za pamoja zilipigwa pamwe na Mheshimiwa Rais Kikwete.

Tafrija ya vinywaji na vitafunwa ilihitimisha sherehe hiyo iliyodumu hadi saa 6 ya usiku.

Bashasha, tabasamu ang'avu, unyenyekevu, haiba na weledi wa mwenyeji wa hafla hiyo, Mheshimiwa Raisi Kikwete, viliongeza maradufu msisimko na mvuto wa hafla hiyo na watu waliondoka bila uchovu, bali wengi wao walijiona kama walikuwa kwenye ndoto ya ujinini.

Ukweli wa Ahmadiyya waingia Kahama

- ***Walimu wa Jamaat wawekwa ndani kwa hila***
- ***Watolewa mahabusu kimiujiza***
- ***Masheikh wa Bakwata Wilaya waomba radhi-tumewasamehe.***

Na Sadr Khuddamul Ahmadiyya Tanzania

Nakumbuka ilikuwa ni safari ya Majlis Khuddamul Ahmadiyya nchini Uganda, ambapo msafara huo uliokuwa na watu thelathini ulisimama katika mji mdogo wa Kagongwa, Wilaya ya Kahama katika Mkoa wa Shinyanga na kama kawaida Khuddam waliingia mitaani na kusambaza vipeperushi na magazeti yaliyokuwa na ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa. Naikumbuka ile jazba iliyotumika kusambaza ujumbe ilikuwa kubwa na kwa muda mfupi sana tuliosimama pale na kwa udogo wa mji ule ilitosha wenyeji kufahamu juu ya msafara wetu. Wakati baadhi yetu wakipata chochote wengine walitumia nafasi hiyo kufanya mazungumzo machache na wenyeji huku wakionyesha



Picha ya Pamoja: Amir na Mbashiri Mkuu (katikati), Rais wa Mikoa ya Mwanza na Shinyanga (kulia) na Rais wa tawi la Sungamile (kushoto).

shauku ya kupokea magazeti na vipeperushi hivyo.

Baada ya kurudi toka nchini Uganda tukapata taarifa kwamba, Mwalimu wetu wa Mkoa wa Shinyanga alipigiwa simu na Imamu wa msikiti wa Sungamile katika Wilaya ya Kahama ambaye anaishi mji mdogo wa Kagongwa kuwa anapenda kujua habari za Ahmadiyya kwa undani. Hapo ndipo ulikuwa mwanzo mzuri wa Jamaat Ahmadiyya kuingia kwa kasi Wilayani Kahama. Vuguvugu la mahubiri lilipamba moto na jazba za watu wa Kahama kumtambua Masihi ilikuwa kubwa kiasi kwamba umati mkubwa wa wafuasi wa kisunni na msikiti wao waliikubali Jamaat Ahmadiyya na kuamua kujiunga nayo.

Baada ya habari hizi, Makao Makuu iliamua kumtuma Mwalimu Abdullah Mbanga aliye mahiri katika Nyanja ya mahubiri na kufanikiwa kufanya mikutano na mihadhara mbalimbali katika kijiji cha Sungamile ambapo wafuasi karibu wote wa msikiti wa kijiji hicho walijiunga na Jumuiya Ahmadiyya.

Majlis Khuddamul Ahmadiyya ambayo kimsingi ilianzisha mwendo kule kahama kwa kauli moja ilimtuma mwanachama wake mahiri Mwalimu Othumani Kingo kwenda Kahama Sungamile na kukaa na wenzetu hawa wapya na kuwapatia malezi, mafunzo na kila aina ya uvumulivu katika uamuzi wao huo mgumu waliouchukua wa kukubali mafundisho sahihi ya dini Tukufu ya Islam.

Katika kipindi ambacho Mwalimu Kingo yupo Kahama kijijini kule Sungamile Waahmadiyya wapya walipata kila aina ya vitisho, bughudha, masingizio, manyanyaso, kutengwa, matusi na vijembe kutoka kwa watu ambao wanajiita ni wakereketwa wa Uislam kutoka Kahama Mjini. Mwalimu Kingo ni mahiri katika malezi kama alivyowahi kufanya kazi hiyo kule Mbeya Jamaat ya Ilongo ambayo alitumwa na Majlis Khuddamul Ahmadiyya, aliwapa moyo na kuwakumbusha subra kwani ushahidi unaonyesha kuwa hatua hizi zinawafika tu wale

Endelea uk. 8

Ukweli wa Ahmadiyya waingia Kahama

Kutoka uk. 7

wenye itikadi ya kweli juu ya dini yao. Kamwe si kazi ya Uislam kujibu mapigo wala kurudi nyuma waila tujiandae na mengine zaidi ya hayo wanayoyafanya kwani nao wanatafuta njia mbalimbali baada ya kukosa hoja.

Nakumbuka Mwalimu Kingo aliwahi kufanya mijadala mbalimbali kule Kahama ambapo waahmadiyya walialikwa na Sheikh wa Wilaya na timu yake. Baada ya kufika ofisini kwao Masheikh hao walikataa mjadala na badala yake kutoa nyudhuru mbalimbali. Hali iliwaongezea jazba waahmadiyya hawa wapya kwani ni aibu kubwa kwa Sheikh kushindwa kutetea imani yake japo kwa dakika chache. Kilichofuata baada ya hapo ni kuanzisha madai mapya kuwa waahmadiyya wameteka msikiti na kutuita kuwa sisi ni Al qaeda. Madai haya na propaganda hii ilianzishwa na watu wa Bakwata pale Kagongwa na kuelekea Wilayani Kahama .

Majlis Khuddamul Ahmadiyya kwa kufanya mawasiliano na Mwalimu Kingo na Mwalimu Kaswezi wa Mkoa wa Shinyanga kwa kushirikana na Waahmadiyya wenyeji walilazimika kuacha kutumia msikiti ule ili isionekane kuwa Ahmadiyya tunagombea msikiti kwani hiyo si tabia yetu pia ni vyema tuache kutumia msikiti ule kwani unaweza kuwa chanzo cha fitna kwa wapinzani wa Jumuiya kama ambavyo walivyoanza kufanya. Waahmadiyya wapya waliendelea kukumbushwa kuwa huo ni mtihani na wapinzani hawa wataendelea kutafuta chokochoko nyingine ili kuipaka matope Jumuiya na Wahmadiyya. Katika kipindi hiki kigumu cha kimalezi na watu kusali majumbani mwao kwa mashaka waliendelea kukutana nyumbani kwa Rais wa tawi aliye mahiri Nd. Shaaban Kalanga angalau siku ya Ijumaa. Fitina iliendelea kuenezwa kuwa Ahmadiyya ni Al qaed ndiyo maana waliteka msikiti, kwa bahati mbaya fitina hii ilipenyezwa kwa wanasiasa, viongozi wa Serikali na Polisi pamoja na kwa watu mashuhuri kuanzia Kahama mjini, Kagongwa hadi kijijini Sungamile. Bila ya kufanya utafiti wa kina watu hawa waliingia kwenye mtego wa fitina za Masheikh na kusahau kabisa majukumu yao na hivyo kuwafanya waahmadiyya pale sungamile wakose mtetezi zaidi ya kumtegemea Mwenyezi Mungu.

Kwa bahati nzuri wananchi wa kawaida walielewa kuwa Waahmadiyya wanasingiziwa kwani aina ya uzushi wanaopewa haufanani na watu hao, pamoja na masingizio hayo waahmadiyya wameendelea kuwa wapole , watiifu kwa Serikali na wanyenyekevu hadi kwa maadui zao. Walikuwa wakiwatembelea wanasiasa kueleza uzuri wa mafundisho ya Islam na kamwe Uislam haufundishi ugaidi, mauaji na kuteka misikiti na Jumuiya hii kamwe haina uhusiano wowote siyo tu na Al Qaeda bali na kikundi chochote kinachoshabikia vurugu hapa duniani. Sisi ni watu wa amani na hapa Kahama tupo Kuhubiri amani ambayo ndiyo Islam ya kweli.

Baada ya tafakuri ya kina kuhusu hali ya Jamaat Kahama, Majlis Khuddamul Ahmadiyya ilipata taarifa ya kuuzwa kwa kiwanja



Ujenzi wa Msikiti wa Jamaat Ahmadiyya tawi la Sungamile ukiwa kwenye hatua za mwisho za umaliziaji

ambacho kingefaa kujengwa msikiti katika kijiji cha Sungamile. Baadhi ya wanachama wa Khuddamul Ahmadiyya walichanga fedha, zilitumwa kwa haraka manunuzi yakafanywa. Hali hii ikafuatiwa na kuanza ujenzi wa msikiti katika hatua ya msingi. Mwalimu Othumani Kingo aliwahamasisha Waahmadiyya wapya kufanya waqar amal na kazi hii ikaisha vizuri.

Wapinzani wa Ahmadiyya hawakukosa la kusema na safari hii walikuja na mpya ni kwamba, hawa watu si waislam inakuwaje wanajenga msikiti mwingine wakati kuna msikiti hapa jirani? La haula wamesahau walivyotukataza tuwapishe kwenye msikiti wao!

Tena wakasema hawa si Waislam kwani wanashabikia ndoa za jinsia moja! Ili muradi wanakuja na jipya kila kukicha. Waahmadiyya waliendelea kukumbushwa kuwa huo ni mwanzo tu wa safari ndefu ya mitihani na masingizio hivyo tukaze mikanda na kumuomba Mwenyezi Mungu awasamehe watu hawa kwani hawajui walitendalo.

Baada ya kupata taarifa ya kina toka kwa Mwalimu Kingo baada ya kurejea toka Kahama, Amir na Mbashiri Mkuu aliagiza kuwa ujenzi huo uendelee na kumtuma Mwalimu mwingine mahiri kusimamia suala hilo. Mwalimu Mohamed Namwete Sudi alitii agizo hilo na mara moja akafika Kahama kwa kazi hiyo. Boma la msikiti lilianza kujengwa kwa kasi kubwa. Maadui hawakubaki nyuma kwani fitina ilipelekwa mbali sana hadi Wilayani Kahama na Kagongwa Polisi, kwamba waahmadiyya hawaruhusiwi kujenga msikiti pale sungamile kwa sababu mbalimbali walizoeleza. Baada ya kupata taarifa hii Amir wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaundry alimuandikia barua Kamanda wa Polisi wa Mkoa Shinyanga na Wilaya ya Kahama yenye maelezo ya kina ya utambulisho wa Ahmadiyya Tanzania na jinsi inavyofanya kazi zake. Amir wa Jamaat alimuagiza Rais wa Jamaat Ahmadiyya wa Mikoa ya Mwanza na Shinyanga kupeleka barua hizo kwa mkono. Wakati hili likiendelea Wakuu wa Polisi wa Kagongwa walivamia kijijini Sungamile na kuwakamata kama wezi Waalimu wa Jamaat Ahmadiyya ambao ni Mwalimu Mohamed Namwete Sudi na Mwalimu Mussa Mohamed Kaswezi. Aidha taarifa zinasema pia walimkamata Rais wetu wa Jamaat Nd. Shaabani Kalanga kana kwamba ni Jambazi na kuwekwa selo ngumu na huku akitishiwa kufukuzwa kazi ya Serikali anayofanya. Wakuu wa polisi wa Kagongwa ambao waliiva kwenye fitina na kusahau kabisa majukumu yao, waliwapeleka viongozi hao wa kidini mahabusu ya Kahama mjini na kulala ndani.

Pamoja na juhudi kubwa za mawasiliano ilishindikana kuweza kuwatoa ndani wenzetu hao mapema kama ilivyotarajiwa na badala yake ni vitisho toka kwa wakuu wa Polisi wa Kagongwa. Ambapo walienda mbali kwa kuwataka walimu wetu wasirudi kamwe Sungamile na Rais wetu aelezwe Mkurugenzi wa Halmashauri Wilaya ya Kahama ambayo ni mwajiri wake ili amfukuze kazi. Ili muradi ni vitisho kwa kwenda mbele.

Rais wa Mkoa wa Mwanza na Shinyanga na msafara wake ulienda kumuona Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga na kumkabidhi barua toka kwa Amir wa Jamaat na kumpatia maelezo ya ziada kuwa, "hivi tunavyoongea waalimu wetu wa dini wapo ndani Kahama Mjini". Baada ya kuelewa hali halisi, Kamanda aligundua kuwa hapo hakuna mgogoro wa kidini ila kuna tofauti za kiimani na jukumu la Serikali ni kuwapatanisha na kuleta suluhu ili kila mtu avumilie imani ya mwenzake. Kamanda alienda mbali zaidi kwa kupiga simu Kahama na kuagiza kuwa hataki kusikia tena suala hilo kwani Jamaat Ahmadiyya imesajiliwa Tanzania kueneza imani yake na pia kutoa huduma za kiroho kwa wafuasi wake ikiwamo kujenga misikiti. Haki hii wanayo Ahmadiyya kama walivyokuwa nayo Bakwata na Taasisi zingine za dini.

Rais wa Mikoa ya Mwanza na Shinyanga na msafara wake walienda hadi Kahama mjini na kuonana na viongozi wa Polisi na hatimaye walimu wetu wakaachiwa bila ya masharti yeyote. Ruhusa ya kuendeleza ujenzi wa msikiti ilitolewa na wenye mamlaka na kukubaliwa kuwa ufanyike Mkutano wa pamoja wa dini zote kwa nia ya maridhiano, hili ndilo tarajio la Ahmadiyya kwani mkutano ule ulifanyika na kuhudhuriwa na Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya kahama.

Wapinzani hawakukaa kimya waliibuka na jipya na safari hii walimtangaza Rais wetu wa tawi la Sungamile ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kijiji Nd. Shaabani Kalanga kuwa si Muislam na hafai kuchinja nyama yeyote.

Kwa fadhila za Allah, Ujenzi umeendelea na kwa sasa msikiti upo katika hatua ya matumizi na hivyo wapinzani hatuwapigi vijembe ila wanapaswa kukumbuka kuwa kokote kwenye ukweli uwongo hujitenga. Hoja zinazoelezwa na Ahmadiyya ukitumia akili kidogo tu utagundua ukweli mtupu unaoelezwa na Islam na hivyo jukumu la kuitetea Islam limebaki kwa Jumuiya ya Ahmadiyya. Aidha Mwalimu Mohamed Namwete Sudi alitembelea Kahama Mjini na kukutana na Sheikh mmoja wa kisuni na kumuomba radhi kwa yote yaliyotokea na yeye hakujua undani wa jambo lenyewe. Mwalimu alitumia fursa hiyo kumpa ujumbe rasmi wa Masihi Aliyeahidiwa na kuahidi mazungumzo zaidi ya kupata elimu.

Wakati naandika makala haya, akaingia Nd. Shaabani Kalanga akiwa ni mjumbe wa Shura toka tawi la Sungamile, Kahama ambapo alinileta hati ya mauziano ya kiwanja hicho cha msikiti. Aidha nilitumia fursa hiyo kumpeleka kwa Amir wa Jamaat ili ajuana naye. Amir Sahib alifurahi sana na kumpa pole kwa mitihani yote iliyomkuta na kumuomba aendelee yeye na wote wa Kahama kuwa wapole na kuonyesha khulka njema ili wapinzani wetu watupende na kuamua kuifuata Jumuiya ya Ahmadiyya. Amir sahib alimwambia sisi Ahmadiyya kamwe hatujibu vurugu zao kwa vurugu bali tunajibu kwa kumuomba Mwenyezi Mungu na kuwa wapole wakati wao wamehamaki na kusema Amani! Amani!. Amir Sahib alimtaka Rais kwa ukubwa wa msikiti huo wana jukumu la kuhakikisha kuwa wanapata watu wengi zaidi ili ujae waumini.

Jukumu letu kama Khuddamul Ahmadiyya ni kuisadia Jamaat ili msikiti huu ufikie malengo yake. Ujenzi wake bado unaendelea na fedha bado zinahitajika, kwa kila Khuddam mwenye kuhitaji kuchangia ujenzi wa msikiti huu naomba sana wasiliana na mwandishi wa makala haya. Kwa picha zinazoenekana inatosha kusema kuwa milango na madirisha bado, minara bado na hatua mbalimbali zinahitajika kufanywa.

Mwisho tunawaomba wapinzani wa Ahmadiyya wasipoteze muda kuizuia kuingia katika mji wowote hapa duniani. Bishara ya Masihi Aliyeahidiwa inasema "nitaufikisha ujumbe wako kila pembe ya dunia". Ni nani atakaezuia? Badala yake tunawaomba kwa unyenyekevu mkubwa watu wote wajiunge na silsila hii ya Ahmadiyya ili kuipa ushindi Islam.

Neno la kuihitimisha ni kwamba 'kila Sifa Njema Anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa Walimwengu'.



TANGAZO

BARAZA KUU LA WAISLAMU TANZANIA BAKWATA
OFISI YA MTA KATA YA ISAGEHE NA MWALUGULU
S.L.P 54 KAHAMA,
TAR 12/03/2014.

YAH: SAHBANI KALANGA KUPIGWA MARUFUKU.

BAKWATA IMEMPIGA MARUFUKU KUCHINJA MBOGA ZA KIJAMII, BW. SHABANI KALANGA KAMA VILE NG'OMBE, MBUZI, KUKU, KONDOO N.K, KWAMFANO;- MSIBA, HARUSI, MGAHAWA, HOTELI, MIKUTANO YA KIJAMII NA KWA WATU BINAFSI. NA MTU YEYOTE AMBAYE MBOGA YAKE ATACHUNJ... A NA BW. KALANGA TUTAHESABU NYAMA HIYO NI NYAMAFU KWA VILE SHABANI SIYO MUISLAMU KWA SASA. MCHINJAJI WETU KWA SASA NI ABDULA PASCALI NDIO ANARUHUSIWA KUVACHINJIA. TUNAOMBA USHIRIKIANO WENU.

WAKALA:-

- MTENDAJI WA KIJIJI S... KWA TAARIFA
- M/K KIJIJI KWA USALAMA
- UONGOZI WA KIISLAMU SUNGAMILE NA VITONGOJI VYAKE KWA UTEKELEZAJI.
- KATIBU KATA MWALUGULU KWA TAARIFA
- MKUU WA KITUO CHA P... SUKAGONGWA KWA TAARIFA
- KATIBU TARAFA ISAGEHE KWA TAARIFA
- SHEKHE WA KAHAMA

...DAMENI
TUNAOMB... USHIRIKIANO WENU
...NDIPAA

SHEKHE WA MKOA BAKWATA KAHAMA KATA ISAGEHE & MWALUGULU

Tangazo ambalo lilitolewa na Uongozi wa Bakwata kata ya Isagehe la kumpiga marufuku Rais wa Jamaat ya Sungamile Bw. Shabani Kalanga ili asichinje wanyama kwa ajili ya kuliwa.

Ndoto 3 tukufu za Mtume Muhammad s.a.w

Ustadhi ***A .R. Mikila – Morogoro***

Kutoka toleo lililopita

NDOTO ZA MTUME MUHAMMAD (SAW).

Majeshi ya makafiri yalirudi Makka bila shangwe wala habari njema ya ushindi. Kimawazo waligawanyika, viongozi walipoteza ushawishi kwa watu wao, hasa katika mipango mingine ya vita. Kwa jumla myoyoni walikiri kushindwa, dhidi ya majeshi ya waislamu kimbinu na kiushujaa. Dhana hii ilitengeneza mdororo wa ujasiri na kujiamini kwa watu Makka. Hofu iliingia katika myoyo ya wale walioshiriki vita hii ya Handaki. Hali hiyo ilipokuwa dhahiri na iliyotanda, ndipo Mwenyezi Mungu (SW) alipo mpelekea Mtume Wake ndoto hii na kumuonyesha akitufu Kaaba.

MAANDALIZI YA KWENDA MAKKA KWA HIJA

Siku chache baada ya kuota ndoto hii ya **Kutufu Kaaba** mwezi Februari 628 Hijiria, Mtume (saw), alijipanga kisafari akiwa na Masahaba 1500 shupavu, tayari kwa safari ya kwenda Makka. Ilikuwa mwezi Februari 628 Hijiri,Mtume (saw) alifunga Safari ya kwenda Makka.

Kutoka Makka kwenda Madina si safari ya siku moja, kwa sababu hiyo baadhi ya watu hasa wanafiki, walipata habari ya azma hii safari na msafara huu wa mahujaji wa kiislamu kwenda Makka, wakiongozwa na Mtume (saw). Wanafiki wakapeleka habari kwa watu wa Makka ya uchochezi juu ya msafara huu, wa Mtume (saw) na Masahaba zake.

Machifu wa Makka walipo pata habari ya msafara huu wa mahujaji waislamu, kutoka Madina, walibabaika sana.Wakatuma vikosi vya wapelelezi njiani, ili kutoa taarifa ya ujio huo. Kwa njia hii viongozi wataweza kufanya mpango wa kuuzuia msafara huu wa Mtume na watu wake, wasiweze kuingia Makka. Mtume (saw), na yeye kwa upande wake alitanguliza kikosi kidogo cha ki-intelijensia kuarifu hali ya usalama wa njia. Kikiosi cha Mtume (saw), kilitoa taarifa kuwa, Maquraish wamejipanga kivita kwenye barabara kuu ya kuingia Makka kwa nia ya mapigano. Katika hali hiyo Mtume (saw), akaamuru msafara ubadili njia yake; wapite njia ya jangwani itakayo wafikisha Makka. Walipita njia hii ya kuelekea jangani, wakasafiri hadi wakafika Hudabiya, hapo wakapiga kambi kwa muda wa siku tatu. Kwa bahati nzuri njia hii iliyowafikisha Hudaibiya haikuwa na kipingamizi chochote. Kama Mtume (saw) na wafuasi wake wangalitaka kuingia Makka kiuvamizi, basi kwa kupitia njia hii wangaliweza kuingia na kuiteka Makka yoyte. Lakini hilo halikuwa lengo la safari yao. Ule ulikuwa ni Mpango wa Allah Mwenyewe kwamba, atuwe Hudabiya kwanza, kisha aombe ridhaa ya watu wa Makka ya kuingia katika mji wao, kwa nia ya kutufu Kaaba. Akisha pata ruhsa hiyo ndipo aingie na kufanya Hija kwa amani na salama yeye na watu wake. Ruhusa ya kuingia Makka ndilo jambo lilo kusudiwa na Allah lifanyike kwanza, kisha ndipo aingie kwa shughuli ya kutufu.

"..(Allah)Alijua msiyoyajua, na kabla ya haya Aliwapeni ushindi uliokaribu" (48:28)

Taarifa hii ya ujio wa waislam katika Haji, uliwasitua sana watu wa Mkka. Walisituka kwa sababu walidhani kuwa Mtume (saw), na masahaba zake wamekuja kupigana, ili kulipiza kisasi cha vita zilizo tangulia, kumbe sivyo. Ni dhana yao tu ya uadui dhidi ya uislam, ndiyo iliyo wasukuma kujipanga kivita na kuwasubiri njiani. Mtume (saw), na masahaba zake walikaa Hudabiya, kusubiri ruhusa ya watu wa Makka, ili waweze kuingia mjini na kutufu Kaaba bila kuhitaji vita.

Machifu wa Makka walipopata habari kuwa, Muhammad na Wafuasi wake wapo katika bonde la Hudabiya. Basi wakamtuma mmoja wa machifu wao aende kuonana na Mtume (saw), na amuulize nini makusudio ya safari yake! Chifu Budaily bin Waraqa ndiye aliye tumwa . Alifika kwa Mtume (saw), akamuuliza madhumuni ya safari yao, Mtume (saw) alimuelezea Bwana Budaily kuwa madhumuni ya safari ile ni kutufu Kaaba. Chifu Budaily alimwambia Mtume (saw) kwamba hilo halitawezekana, hawampi ruhsa kuingia Makka. Iwapo atatumia nguvu, ajue kuwa yeye analo jeshi la kumzuia kivita asiingie Makka kutufu Kaaba. Mtume (saw), alimwambia Budaily kwamba mapigano yanini? Vita hazijawahi kuleta manufaa yeyote kwa Maquraishi, pamoja na kwamba wamepigana kwa miaka nenda miaka rudi. Turuhusuni tuingie hata kwa mapatano maalum ya kuacha mapigano, kwa faida ya pande zote mbili. Chifu Budaily aliona wazo hili la kuingia mapatano ni zuri na jema; akarudi na kuwaambia watu wake.

Habari hii ikaenea kwa Machifu wengine wa Makka. Wengi waliupenda na kuuafiki ushauri huu. Lakini wakasema, makubaliano hayo yawe ya kuandikiana, na bila kumruhusu yeye na wafuasi wake kuingia Makka kutufu Kaaba mwaka huu. Kama ni kutufu, basi mkataba useme



Ustadh Abdulrahman Mikila

wazi wazi kuwa ruhusa hiyo inaanzia mwakani na kwa masharti ya kutoingia Makka na silaha za kivita.

Baada ya mashauriano ya machifu wote wa Makka, ndipo walipo mtuma Chifu Suhail bin Amri kwa niaba yao, kwenda kuonana na Mtume (saw) na kuandikishiana naye mkataba. Baadaye ilikuja julikana kwamba Machifu wale walikataa kuwarusu waislamu kuingia Makka na kutufu mwaka ule, kwa sababu waliogopa fedheha mbeleya watu wao. Kwa vile kabla ya ujio huu wa ghafla wa Mtume (saw) pamoja na watu wake, mengi ya majigambo ya nguvu zao waliyasema na kujiapiza kwingi dhidi ya waislamu. Kwa sababu hiyo waliona watumie ushupavu tu usiyo na mantiki, wa kukataa kutoa ruhusa hadi mwakani kuficha aibu zao.

Mtume (saw), kwa upande wake alimtuma Sayidina Uthmani (ra), kwenda kuongea na Machifu wa Makka, kuomba kibali cha wao kuingia Makka kutufu Kaaba. Maongezi yale yalichukua muda mrefu kiasi cha kusababisha uvumi kwamba, Uthmani (ra) ameuawa. Kwa taarifa hizo za kuudhi, Mtume (saw), akasema iwapo habari hii itakuwa ni ya kweli, basi hatuna cha kungoja tunalazimika kupigana na kuingia Makka kinguvu; kulipiza kisasi cha kuuawa mjumbe wetu. Hapo Mtume (saw) akaamuru shime ya Masahaba kujitolea kwa vita ya kulipiza kisasi, kwa ahadi ya kupigana bila kurudi nyuma hadi ushindi upatikane. Ahadi hii maalumu iliyochukuliwa chini ya mti kule Hudaibiya; ndiyo iliyo kuja julikana kwa jina la **Baiyatu Ridhuwan**.

Kwa bahati nzuri kabla masahaba hawa, hawajamaliza kula viapo vyao vya utii, kwa kuwekewa mkono wa Mtume (saw) juu ya mikono yao, mara Sayidina Uthmani akatokea akiwa salama salimini; hapo vita ikaakhirishwa. Kufika kwa Sayidina Uthmani kukawa sambamba na kufika kwa Chifu Suhail bin Amri, kiongozi wa watu Makka. Alipo fika chifu Suhail akasema: " nimekuja kufanya mkataba na Muhammadi".

Maelezo ya mkataba huo na masharti yake, yamebainishwa vizuri katika kitabu cha Maisha ya Mtume (saw) kilicho andikwa na Khalifa wa Pili wa Masihi Aliye ahidiwa Hadhrat Mirza Bashirud-din Mahmuudi Ahmad (ra).

Ndoto hii ya kujiona anatufu Kaaba, ndiyo iliyo mfanya Mtume (saw) afunge safiri yeye pamoja na Masahaba zake, kwenda Makka, na hatimaye wakaishia Hudaibiya, kwa kuwekeana Mkataba na Chifu Suhail kwa niaba ya watu wa Makka wa kuacha mapigano kwa muda wa miaka kumi na kutoa ruhusa kwa Waislamu kuingia Makka kufanya Haji.

FAIDA YA MKATABA WA HADAIBIYA

Faida kubwa zilizo patikana kutona na mkataba ule ni hizi:-

1- Mtume (saw) na wafuasi wake pamoja na watu wa madina kwa upande mmoja, na watu wa Makka kwa upande wa pili waliweza kupata matumaini ya kuwa na kipindi cha amani na utulivu cha miaka 10 bila vita.

2- Kupitia mkataba huu, ruhusa ya kupata washirika na marafiki, ilitolewa kila upande na kila kabila lilipewa hiyari ya kuchagua mshirika amtakae.

3- Mkataba uliwaruhu waislamu wa Madina kufika Makka, kadhalika watu wa Makka kufika Madina kwa uhuru.

4- Baada ya mkataba huu, watu wengi walipata fursa ya kujiunga na dini tukufu ya islamu kwa uwazi na uhuru zaidi. Watu maarufu, kama kina Khalid bin walidi bin Mughira, Uthmani bin Talha na Amri bin Al'asi wa baniy Sahmi wote hawa walijiunga na uiaslamu mwaka mmoja tu, baada ya mkataba huu. Makabila kadhaa yakaunga urafiki na dola ya kiislamu.

5- Kupitia fursa iliyopatika ndani ya mkataba huu, Mtume (saw) aliweza kuwaandikia barua wafalme wa nchi mbali mbali kuwataka binasfi, wao pamoja na rai zao wajiunge na dini ya Islamu.

6- Mkataba huu, ndiyo uliyo mtikisa Abu Sufiyani kule Damasqas. Alipoitwa katika Ikulu ya Kaisari Mjini kuhojiwa, chini ya ulinzi mkali na kwa masharti ya kusema kweli mtupu. Alijiona kama mtuhumiwa wa mashitaka makubwa.

7- Mwaka mmoja baadae, Mtume (saw) pamoja na Masahaba 2000, waliweza kusafiri bila bughudha kwenda Makka kutufu Kaaba kwa salama na amani.

8- Mkataba huu, ulipo vunjwa na watu wa Makka, uliwawezesha waislamu kuingia Makka kwa kishindo na kuuteka mji wote. Huo ukawa ushindi mkuu wa dini ya Islamu, uliozaa ushindi juu ya ushindi wa bara Arabu yote na nje ya mipaka.

Kauli ya Allah juu ya ndoto hizi ni hii:-

"Yeye Ndiye Aliye mtuma Mtume wake kwa muongozo na dini ya haki, ili Aishindishe juu ya dini zote na Allah Hutosha kuwa shahidi"(Kur 48:30)

Nimalizie kwa kusema kuwa, ndoto zote hizi tatu zaMtume Muhammadi (saw) nilizo zielezea zilikuwa sawa na ramani ya njia kuelekea kwenye ushindi na ustawi wa dini ya Islamu. Ramani hiyo ilikuwa inachorw kuonyesha umbali wa kila kituo kuelekea ushindi mkuu waislam . Kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine kilikuwa na umbali wa miaka miaka mitano. Katika kila kituoni utakutana na matukio makuu. Kadhalika ndoto hizo zilitabiri muda na wakati wa kufika katika kila kituo, ili kuelekea ushindi kamili. Miaka mitano ya kwanza ilipopita baadhi ya waislamu walihamia Ethiopia. Baada ya miaka mitano mingine, waislamu walihamia madina. Mwaka wakumi na sita waislamu wakaiteka Makka na kuifanya bara Arabu yote kuwa chini ya himaya ya Mtume Muhammad (saw). Hizi ndizo hatua za kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine. Uislamu ulishinda na Makkafiri wa Makka pamoja na marafiki zao walishindwa.

UISLAMU CHINI YA BENDERA YA MASIHI ALIYE AHIDIWA

Bendera ya ushindi wa dini ya islamu katika zama hizi ipo mikoni mwa Jumuiya ya waislamu wa Ahmadiya. Jumiya hii iliasisiwa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmadi (as) mwaka 1889, kazi yake kuu ni Dai Ilallah. Ewe muislamu unaye itakia mema dini hii tukufu ungana na kikosi kazi hiki cha Masihi na Mahdi aliye ahidiwaili na Mtume (saw), nawe uchangie katika ushindi wa hoja siyo wa vioja.

Mwenyzi Mungu Amemuahidi Mtume wake kuwa uislamu utashinda kwa mara nyingine na wa pinzani wake watashindwa vibaya. Inshaallah.

Kisoma uelimike, asaa utadhukuri,
Kizacho kikuondoke, nguvu ni zake Kahari,
Ufalme wote Wake, wa Ardhi hata Dari.
Kama hujapata fungu, Mungu atakukirimu.

Mwisho

Barua ya Msomaji

ZAWADI KWA WA-AHMADIYYA; MAJIBU YA HOJA ZA ENG. K. S. KAZEMA.

Ndugu Mh. Eng. K.S. Kazema,

Kwanza kabisa nimshukuru Allah na nimtakie Rehma na amani, kipenzi cha Allah, Mtume Muhammad (S.A.W). Amabaada ya kumshukuru Allah. Nilumie fursa hii kumpongeza Mh. Eng. Kazcma kwa mada yake aliyoitoa kuhusu kuendelea kwa utume katika gazeti la Mapenzi ya Mungu, la Mwezi wa Nne, 2014, wakati akijibu hoja za aliyemuita Salehe Abdul wa Morogoro, nasema aliyemuita kwa sababu ametuwekea majibu yake tu, pasina kuweka hoja za huyo ndugu ili wasomaji tupate kulinganisha hoja, hivyo basi kutufanya wengine tunaofikiria na kutazama mbele kidogo tutambue kuwa pengine, ametunga hoja mwenyewe na kudai anamjibu ndugu aliyemtaja kwenye gazeti kama ilivyokuwa kawaida ya wa-ahmadiyya kuendesha dini kwa propaganda badala ya ukwdi halisi. Lakini pamoja na hayo ningependa pia nitumie wasaa huu, kuzijibu hoja zake moja baada ya nyingine kadri Allah atakavyonijalia, na naomba kama kweli wa-ahmadiyya mnaamini dini yenu ni ya kweli kutoka mioyoni mwenu, mziweke hoja hizi kama zilivyo kwcnye gazeti lenu la Mapenzi ya Mungu halafu mzijibu kupitia gazeti hilo hilo ili wasomaji wapate kuchambua wenyewe ni upi mehele ni ipi pumba.

Ama baada ya utangulizi huo, ningependa nianze na hoja ya kwanza ya ndugu Eng. Kazema, aliyoitoa wakati akijaribu kuthibitisha kuwa Bwana Yesu hakupaa, mbinguni. Ushahidi alioutoa ukiwa ni wa kwanza kabisa kuthibitisha ukweli wa hoja zake ameutoa ndani ya b*iblia "hakuna atakayepaa mbinguni ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni"*, kwa kifupi jambo hili limenishangaza sana na limekuwa likinishangaza na kunichefua mno, pale ninapoona watu wanaodai kuwa ni waislam wanatafuta ushahidi wa kuthibitisha ukweli wa jambo ambalo linawatatiza waislam kwa kutumia biblia.

Ndugu, Kazema, na ndugu wa-ahmadiyya, jambo hili ni kinyume kabisa na mila za kiislam, kwani Allah anasema wanapotofautiana waislam suluhisho ni kurudi kwa Mwenyezimungu na Mtume wake na hatukuambiwa turudi katika maandishi ya Biblia kama ndugu zetu mnavyojaribu kufanya. Lakini kwa kuwa elimu ni pana kama lipo andiko ambalo pengine Allah au Mtume Mtukufu alisema wanapotofautiana waislam, basi warudi kwenye biblia ningependa ndugu yangu na kaka yangu katika taaluma Eng. Kazema atuoneshe labda pengine ni uchache wangu wa elimu ya dini ndio unaonifanya nisitambue hilo.

Lakini pia, biblia ni kitabu ambacho Mirza Gulam mwenyewe zaidi ya mara moja amekuwa akisema kuwa ni kitabu kinachoongoza watu kwenye njia ya upotofu, lnashangaza sana kuona leo wafuasi wake wanakitumia ili kupata hoja, kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao ya kiroho, huku wakisahu na kuyadharau maneno ya wanayedai kuwa wanamfuata.

IMANI YA KUNYANYULIWA MBINGlINI;

Ndugu Eng. Kazema, Imani hii sahihi ya Islam ya kunyanyuliwa mbinguni kwa nabii Eisa as inapingwa na wa-ahmadiyya kwa nguvu zao zote na mojawapo ya hoja wanazozitoa kuthihitisha madai yao haya, ni pale wanapohoji kuwa neno hili "kunyanyuliwa mbinguni" halijatajwa sehemu yoyote katika Kuran Tukufu, na hasa wanahoji neno hili "mbinguni" limetoka wapi? Ili hali Quran tukufu inasema alimnyanyua kwake tu na wala haikutaja neno mbinguni?

Ndugu wa-ahmadiyya, neno mbinguni ni kweli kabisa halijatajwa katika Quran au hadithi yoyote, lakini kwa sabahu Allah yeye mwenyewe yupo mbinguni kama anavyoeleza katika Quran;
QURAN SURA AL-MULK 67:18. *"Au je! mnadhani mko salama kwa Aliyoko mbinguni ya kuwa Yeye Hatawapelekeeni kimbunga chenye changarawe? Basi karibuni mtajua lili-vyo onyo Langu."*

Kwa hiyo ndugu zangu wa-ahmadiyya, kwa mujibu wa Aya hiyo Allah yuko mbinguni na Arshi yake imetanda kote na ni vyake vyote viliomo mbinguni na Ardhini. Kwa hiyo Allah aliposema kuwa "alimnyanyua Issa kwake" maana yake ni kwamba alimnyanyua kwake mbinguni. Aya hii pia inavunja imani yaw a-ahmadiyya kuwa Allah hana makao maalum, hapana Allah yuko mbinguni isipokuwa uwezo wake juu ya kila jambo upo kila mahala, mbinguni na ardhini.

IMANI YA MIRZAH GHULAM JUUYAISSAKUNYANYULIWA MBINGUNI;

Ndugu Eng. Kazema, ndugu wa-ahmadiyya, Mirzah Ghulam ambaye nyie mnadai kuwa wafuasi wake, anapingana kabisa na imani yenu hii isiyokuwa ya kiislam, kuwa Nabii lssa hakunyanyuliwa mbinguni, kwani Mirza Ghulam mwenyewe anaungana na waislam kuamini kuwa nabii lsa alinyanyuliwa mbinguni kama anavyosema katika kitabu chake cha Ushindi wa Islam;

"Lakini kwa kuwa mifupa haikuvunjwa, hivyo akasalimika kwa msaada wa mtu mwema mwenye kumwamini na baada ya kuishi siku zilizosalia za maisha yake, akanyanyuliwa mbinguni." .(Fat-h-e-islam,UK.13)

Ndugu Eng. Kazema, hapa Mirzah Gulam mwenyewe anatuthihitishia kuwa baada ya Nabii Issa kuishi siku zilisolia za maisha yake alinyanyuliwa mbinguni, kwa maana hiyo mpaka sa hizi ninapoandika makala hii, kwa maelezo haya ya Mirzah Gulam, Nabii lssa bado yuko mbinguni, baada ya kuishi siku za maisha yake hapa duniani.

Ndugu, Eng. Kazema, lakini pia ni bora kwanza kabla hujawauliza waislam, neno mbinguni walilitoa wapi pale wanapaelezea kunyanyuliwa Issa na ili-hali kwenye Quran na hadithi halipo, basi ingekuwa bora zaidi kwanza swali hilo ungemuuliza Mirzah Gulam, neno 'mbinguni' alilitoa wapi na ili hali halijatajwa popote. Kwa swali hili inathibitisha uchache wa elimu ya wa-ahmadiyya si katika dini bali hata elimu ya vitabu vya Mirza Ghulam mwenyewe.

USHAHIDI WA QURAN *JUU* YA UHAI WA NABII ISSA;
Kuhusu upande wa Quran, kwa hakika si *jambo* la msingi kabisa kubishana juu ya uhai wa Issa as kwa maana Quran imeeleza katika aya nyingi kinagaubaga kuwa nabii Issa *badu* yu hai aidha tutaonekana watu tusiojitambua iwapo tutaendelea kuwa na mashaka juu ya jambo hili, kwani Allah mwenyewe ameeleza kiasi hiki kwamba hakuna yeyote anayeweza kubaki na mashaka; Kwa leo ningependa niweke mbele aya moja tu ambayo kwa hakika inavunjilia mbali imani ya wa-ahmadiyya juu ya kifo cha nahii Issa; Allah (S.W) anasema;

QURAN SURA AN-NISAA
4:160 "Na hakuna yeyote katika watu wa kitabu ila atamuamini kabla ya kifo chake. Naye (Masihi) siku ya kiyama atakuwa shahidi juu yao."

Ewe ndugu yangu mu-ahmadiyya, hapa hutakiwi kabisa kubaki na chemhe ya wasiwasi kwani Allah anasema, watu wote wa kitabu watamuamini Issa ibn Mariam kabla hajafa. Sasa kama wapo watu mpaka leo wanaamini nabii Issa alikufa ni wazi wanapingana na kauli hii ya Allah na badala yake wanaunga hoja na kauli za mayahudi wanaodai Issa as alikufa.

Tafsiri ya Ahmadiyya juu ya aya hii;
4:160 "Na hakuna yeyote katika watu wa kitabu ila ataliamini kabla ya kifo chake. Naye (Masihi) siku ya kiyama atakuwa shahidi juu yao."

Kwa kuwa wa-ahmadiyya wamesutwa sana na aya hii, wameamua kutoa tafsiri mbovu ili kukidhi haja *zao* za kuupotosha umma wa kiislam, tafsiri waliyoitoa haiendani kabisa na kile kinachozungumzwa katika aya yenyewe, kwa sababu hata mtu ambaye hajui Kiswahili kweli hawezi akasema *"ataliamini kabla ya kifo chake"*, halafu bila kueleza ni linini hilo ambalo wataliamini, kwa mtu anayejua Kiswahili bila shaka atagundua kuwa pengine waliotafsiri walikuwa hawajui aidha Kiswahili au kiarabu vizuri, kwa sababu mpangilio wa kisarufi walioutumia haukubaliani kabisa na lugha zote mbili,ok, tunajua "Nabii Issa ni Neno la Allah" labda pengine wafasiri wa Quran hii walitaka kumaanisha wataliamini neno hili kabla ya kifo chake, kama ndivyo walitaka kumaanisha basi haitakuwa kosa kubwa kwao, lakini kwa neno *"la yu-uminanna bihi"* lililotumika kwenye aya hii, tafsiri yake ni "watamuamini" na si "wataliamini" kama wa-ahmadiyya wanavyojaribu kukwepa kusutwa na maneno ya Allah.

MAONI YA WA-AHMADIYYA JUU YA AYA HII;

Pamoja na kuwa wa-ahmadiyya wameona, nongwa kuweka tafsiri halisi ya neno "layu-uminanna bihi" katika sherehe ya aya hii katika tafsiri ya Quran yao, wamejirudisha kule kule kwani wameandika hivi;
"Sisi tunashauri ufumbuzi ambao ni tofauti na ni MPYA KABISA juu ya tatizo hili. Aya hii inayochunguzwa inatafsiriwa hivi: 'Hakuna hata mtu mmoja miongoni mwa watu wa Kitabu ila bila shaka atamwamini kabla ya kifo chake'. Neno mmoja halikutajwa kwa njia ya kuandikwa katika aya hii bali limedokezwa tu. Kama lingalitajwa basi aya hii ingesomeka kama ifuatavyo: Wa in ahadun min ahlil Kitaabi. Neno ahadun ndilo neno lililodokezwa. Tunashauri kwamba badala ya neno linalodokezwa kuwa ahadun tungelichukulia neno fariiqun kuwa ndio neno lidokezwalo. Kwa hali hiyo tafsiri ingepaswa kuwa hivi" HAKUNA MADHEHEBU AU KUNDI LO LOTE KUTOKA KATIKA WATU WA KITABU ILA LITAMWAMINI YEYE (YESU KRISTO) KABLA YA KIFO CHAKE." (UK. I93, Quran Tafsiri ya Kiswahili ya Ahmadiyya)

Ndugu Eng. Kazcma, ndug M-ahmadiyya, kwa mujibu wa maelezo ya wa-ahmadiyya Katika, maneno niliyoandika kwa herufi kubwa juu inaonesha wazi kabisa kuwa wanakiri kuwa wao wamekuja na UFUMBUZI MPYA KABISA, wa tafsiri ya aya hii, Jambo hili ni la kushangaza sana na linatia aibu pia kuona Mtume amekemea sana watu kuleta mambo mapya katika dini, lakini wenzetu wanafanya bidii kubwa kuleta ufumbuzi mpya katika tafsiri ya maneno ya Allah, jambo hili ni chukizo mbele ya Allah na kufanya hivyo ni zaidi ya kuitwa kafiri, kwa ujumla hakuna jambo jipya katika dini bali kila jambo Allah ameshalieleza na hakuna yeyote anayeweza kujitamba kuwa kaleta ufumbuzi mpya wa tafsiri ya maneno ya Allah.

Hata hivyo, katika maelezo yao niliyoyaweka kwenye herufi kubwa chini, yanaonesha kabisa kuwa waliyokuja nayo si ufumbuzi mpya kama wao walivyojitapa huko juu bali ndiyo tafsiri hasa sahihi ya aya hii, ya kwamba watu wote wa kitabu watamuamini nabii Issa (a.s) kabla ya kifo chake.

Ndugu zangu wa-ahamadiyya tafsiri hii ambayo hata nyie pia mmeikubali inavunja kabisa imani yenu na hoja zenu zote ambazo huwa mnazitoa kwa kuunga-unga Aya za Quran ambazo baadhi kwa asili yake ni "mutashahihat" yaani aya zenye maana nyingi, ili kudanganya waislam kuwa nabii Issa amekufa, bali aya hiyo kwa uwazi kabisa inaonesha kuwa nabii Issa hajafa na yuko hai hadi leo, kwa sababu sote ni mashahidi kuwa tokea Nabii Issa amezaliwa mpaka leo hii, madhehebu nyingi za watu wa kitabu ambazo bado **zinampinga na kumkataa, haijawahi** kutokea katika historia siku ambayo madhehebu yote ya watu wa kitabu yaani Mayahudi na **wakiristo wakamuamini Seyydna Eiza ibn Mariam, hii inathibitisha kabisa kuwa kifo chake** bado hakijatokea kwa sababu mojawapo ya alam aya kutokea kifo cha Nabii Issa ni lazima m**adhehebu yote ya watu wa kitabu wamuamini, na siyo maana yake kwamba wamuamini kama** baadhi ya watu wa kitabu wanaodai kumwamini huku wakimwita Mungu, la bali hata hao wapo kwenye kundi la watu ambao hawajamuamini pia, bali kumuamini kunakosemwa na ayah ii ni kuamini kuwa yeye ni Mtu, na alikuwa ni mtume wa Allah tu na si zaidi ya hapo. Lakini pia hadi leo wapo mayahudi ambao wanamuamini Nabii Musa tu, lakini hawamuamini nabii Issa, sasa tutawezaje kupata ujasiri wa kusema Eisa as amefariki?

Ewe ndugu Eng. Kazema, enyi ndugu Wa-ahmadiyya, kama kweli tuamini kama mnavyosema, kwamba Nabii Eisa mnazareti amefariki, na pia

Endelea uk. 11

ZAWADI KWA WA-AHMADIYYA; MAJIBU YA HOJA ZA ENG. K. S. KAZEMA.

Kutoka uk. 10

kwa kuwa anayedaiwa kuwa nabii Eisa Mqadiani na yeye amekwishafariki zamani za mwaka 1908, hamuoni kuwa ni ushahidi tosha wa kuthibitisha uongo wa imani yenu? Kwa sababu sote ni mashahidi na Allah pia ni shahidi wa kwanza kuwa watu wa kitabu bado hawajamuamini Nabii Issa, japokuwa amekwishakufa tena mara mbili kwa mujibu wa imani ya wa-ahmadiyya. Je ni kwa namna gani manabii Eisa wote wawili wafe halafu watu wa kitabu bado wawe hawakuwaamini? Inamaana mnataka kutuambia bishara hii ya Allah haikutimia (Mungu Apishe mbali kabisa) Hapo labda mtafute uwongo mwingine lakini Allah ameeleza kwa uwazi kabisa, hakika Nabii Eisa hatakufa mpaka watu wote wa kitahu wamuamini.

JE, UTUME UNAENDELEA?

Ndugu, Eng. Kazema, ndugu wa-ahmadiyya, Kuhusu suala la utume kuendelea au kutokuendelea kwa upande wangu mimi huwa sioni kama linastahili kujadiliwa kabisa, bali huwa naona ni kupoteza muda tu ambao tungeutumia pengine kujadili mambo mengine kuhusu Islam kwani jibu liko wazi kuwa Milango yote ya utume ilishafungwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) na hakuna Mtume ajaye baada yake, Lakini kwa kuwa kwa ajili ya ubishi na ugumu wa kuukubali ukweli huu, walio nao ndugu zetu wa-ahmadiyya, mimi naona si vyema kuwaacha waendelee kupotea bila walau kuwakemea, kwani ni jukumu langu kuamrisha mema na kukataza maovu kama muislam. Kwanza kabisa Ningependa nithibitishe jambo hili kupitia maneno ya Mtu wanayedai, kuwa ndiye mtume wao.

Ndugu Eng. Kazema, Ndugu wa-ahmadiyya, Mnamo tarehe 2/10/1891 baada ya Mirzah Gulam Ahmad wa Qadian kushindwa vibaya kwa hoja na Maulamaa na mashekhe wa kiislam alitoa tangazo, ambalo pia lilichapishwa katika kitabu cha *Din-ul-Haq* kilichotungwa na Mir Qasam Ali ambaye alikuwa ni mfuasi na mwanafunzi wa Mirza Gulam mnamo mwaka 1910, yaani miaka miwili baada ya kifo cha Mirza Gulam. Katika tangazo hilo Mirza Gulam alisema;

"Nimesikia baadhi ya Maulvis wa mji huu wa Delhi wakitoa shutuma hizi dhidi yangu, kwamba mimi nimedai Utume, nimekataa uwepo wa malaika na mbingu na moto (wajehannam) na pia uwepo wa malaika jibril na lailat-ul- Qadri na miujiza na kupaa mbinguni kwa Mtume wetu mtukufu. Hivyo basi ili ukweli udhihirike, ninaapa mbele ya wasomi na wasioujua kusoma kuwa madai haya ni ya uongo. Mimi sidai utume, na wala mimi si mkataaji wa miujiza, malaika, lailat-ul-Qadri n.k. Kwa maana nyingine ninaamini katika mambo yote hayo yaliyo katika imani ya Islam, kama wanavyoamini Ahl-i-Sunnat-wal-Jamaat, ninakubaliananla mambo yote haya ambayo msingi wake ni Quran na Hadithi; Na naamini kuwa yeyote atayedai unabii na Utume baada ya Bwana na Mwalimu wetu Hazrat Muhammad Mustafa, rehema na amani za Mungu juu yake, kuwa ni muongo na kafiri. Ninayo imani thabiti kwamba ufunuo wa kwanza wa utume ulishuka kwa Hazrat Adam Safiyy Allah na ulikoma kwa Mtume wa MUngu Muhammad Mustafa, rehema na amani za Mungu juu yake. Kila mmoja na awe shahidi kwenye maandishi yangu haya, na Mungu Mjuzi na Msikivu ni wa kwanza kushuhudia"

MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA TANGAZO HILO;

1. Mirza Gulam anaamini mambo yote kama wanavyoamini ahl-ul-sunnat wal jamaa, yaani kuhusu malaika, miujiza, lailatul qadri n.k, kwa kifupi imani kama ya ahl-ul-sunnat wal jamaat, hii ni tofauti kabisa na Imani ya wale wanaojiita wafuasi wake ambao ni wapinzani wa kila imani ya ahl-ul-sunnat wal jamaa.
2. Mirza Gulam anaamini ufunuo wa utume na unabii ulianzia kwa nabii Adam na kuishia na Mtume Mtukufu (S.A.W), kwa kifupi anaamini utume umekoma, na hauendelei, tofauti na ilivyo imani ya wanaodai kuwa wafuasi wake wa leo, ambao wanaamini utume unaendelea.
3. Mirza Gulam, anaamini yeyote atakayedai unabii na Utume unaendelea baada ya Mtume Mtukufu (S.A.W) ni muongo na kafiri, hivyo hii inatuthibitishia moja kwa moja kuwa kwa ulimi wa Mirza Gulam mwenyewe wa-ahmadiyya wote ni makafiri.

JE QURAN INASEMAJE KUHUSU ISSA A.S KUNYANYULIWA MBINGUNI;

Ndugu Eng. Kazema. Ndugu wa-ahmadiyya kwa ujumla na kwa kifupi kabisa Quran imetaja katika baadhi ya surat kuwa nabii Issa alinyanyuliwa akiwa hai, na siyo baada ya kufa kama wa-ahamdiyya wanavyojaribu kupotosha ukweli; kwa leo kwa sababu lengo langu ni kumjibu ndugu Eng. Kazema naona bora niigusie aya moja ambayo ameijengea hoja kutoka surat Al-imran.

Quran 3:56 *Na kumbuka Mwenyezimungu aliposema ewe Issa hakika mimi nitakufisha na nitakunyanyua kwangu* "

Kwa aya hii wa-ahmadiyya wanaamini inaonesha kuwa nabii Issa alikufa kwa sababu neno liliotumika pale ni "mutawaffiika" kwa ujumla ninashindwa kuelewa ni kwa kigezo gani wa-ahmadiyya wamekitumia kulitafsiri neno hili kufisha, kwa maana ya kufa kwa kutokwa na roho, na ili hali neno hili "kufisha" kwa ushahidi wa Quran yenyewe ni neno lenye maana nyingi.

Lakini kwa kuwa Quran inajitafsiri nitaweka baadhiya surat ambazo neno hili limetumika ndani ya Quran na wa-ahmadiyya hao hao wamelitafsiri kwa maana isiyokuwa ya kufa, kwa mfano; *QURANSURA* 6:61. *"Naye ndiye Anayewafisheni wakati wa usiku, na Anayafahamu mnayoyatenda wakati wa mchana, kisha Yeye Huwafufueni humo* ili *mudauliowekwa umalizike; kisha Kwake marudio yenu, ndipo Atawaambien iyale mliyokuwa mkiyafanya"*

Katika Aya hiyo hapo juu, neno "tawaff' yaani kufisha, limetumika pia lakini hapo likimaanisha maana nyingine kabisa tofauti na kufa, moja kwa moja, bali Mwenyezimungu amelitumia neno hili akimaanisha 'usingizi';

Lakini pia katika Quran tafsiri ya wa-ahmadiyya katika aya nyingine lilipotumika neno"tawaff", ni katika sura ya Az-zummar ambapo Allah *anasema"Allahuyatawaffa-l-anfus"* Wa-ahmadiyya wameitafsiri hivi;

QURANSURA 39:43. *"Mwenyezi Mungu 'Huzichukua' roho za viumbe..... "*

Kumbe pamoja na ubishi wote huo, wa-ahmadiyya wanajua wazi kabisa kwamba neno "tawaff" maana yake pia ni "kuchukua", na/au "kusinzia" sasa kama hivyo ndivyo ni kwa nini basi neno hilo linapotumika kwa Nabii Eisa as wanataka kujifanya hawazitambui maana hizo?

Ndugu wa-ahmadiyya, kwa kuwa neno"tawaff' lina maana nyingi, na kwa kuwa Nabii Eisa hakufa, ni lazima pale Mwenyezi Mungu aliposema"Yaa *Eisa inni mutawafjika, wa rafiuka illayya"* , ni lazima ieleweke kuwa tafsiri ya Aya hiyo ni aidha hii hapa *"Ewe Eisa hakika mimi nitakuchkua, na nitakunyanyua kwangu….."* au iwe hii hapa *"Ewe Eisa hakika mimi nitakupa usingizi na nitakunyanyua kwangu"* kwa tafsiri hizo ambazo kwa jinsi wa-ahmadiyya walivyolitafsiri neno hili "tawaff" katika Aya za 6:61 na 39:43, ninaamini kabisa kuwa wa-ahmadiyya watakubaliana na tafsiri za aya hiyo ya *3:56* nililizoziweka kuwa ni sahihi zaidi, kuliko wanavyojaribu kupotosha ukweli.

JE MIRZAH GHULAM ANAIELEWAJE 3:56 KATIKA QURAN?

Wa-ahmadiyya wanaamini kuwa Mirzah Gulam ndiye aliyepewa funuo, zenye tafsiri halisi ya Quran tukufu, kalika kitabu chake kinachoitwa tadhkirah, Mirzah Gulam ameandika kile anachokiita ufunuo;

"Ewe Ahmad, Mungu amekubariki, hukutupa ulipotupa bali ni Mungu aliyetupa.Ni Rahman aliye(ku) fundisha Quran ili uwaonye watu ambao baba zao hawakuonywa ili njia ya wakosefu ibainike. "(Tadhkira UK.43)

Ndugu Eng. Kazema, naamini kabisa na wewe unaamini kuwa Mirza Gulam alikuwa anapokea funuo ambazo zilikuwa zinatafsiri kile kilichoandikwa ndani ya Quran takriban, miaka 1200 kabla ya kuzaliwa kwake;Mirzah Gulam alidai kuwa maelezo yenye tafsiri sahihi ya Quran alikuwa akiyapokea kupitia funuo zake za Barahain-e-Ahmadiyya na kuhusu aya hiyo amesema;

"Tena mwishoni katika Barahein -e-Ahmadiyya uk.556 habari ya kuzaliwa Issa aliyekuwemo katika tumbo la Mariam imekuja katika ufunuo huu;" Yaa Issa inni mutawaffiika warafiuka ilaiya ..... " Katika ufunuo iluu nimeitwa kwa jina la Issa (Kishti-e-Nooh, UK.32)

Katika kitabu hiki, Mirzah Gulam anaeleza kuwa ufunuo alioupokea kakika Barahain-e-ahmadiyya, unamueleza kuwa maneno haya "Ewe Issa hakika mimi nitakufisha, na nitakunyanyua kwangu... "yeye ndiye Eisa aliyetajwa hapo; na siyo yule Eisa mnazaret tunayemfahamu, tofauti na imani ya wa-ahamadiyya wa leo, wanapokuwa wanatoa maana ya aya hii, wao hudai inamhusu Nabii Eisa Mnazareti, hii inaonesha ni ufinyu kiasi gani wa elimu ya vitabu vya Mirza Gulam waliyonayo wa-ahmadiyya, la sivyo wanaona aibu kuzitumia hoja za mtu wanayemuita nabii wao, hasa wanapokuwa wanajadili, badala yake wanatunga mafundisho yao mengine;

Ndugu Eng.Kazema, Mirza Gulam, ili kuonesha kuwa maana ya maneno ya aya za Quran haipingani kabisa na zile tafsiri alizopokea katika Barahain e Ahmadiyya anasema;

Kurani ipo someni na someni upande mwingine Barahain-e-Ahmadiyya, kasha fikirini kwa uadilifu na akili kwa kumuogopa Mungu ….." (*Kishti-e-Nooh UK.33)*

Kwa maneno hayo Mirza Gulam anawaambianyiewa-ahmadiyya mkitaka kujua tafsiri ya Quran someni Barahain e Ahmadiyya, na mkishaisoma mtagundua kwamba 3:56, Haimuhusu kabisa Eisa Mnazareti;

Lakini Pia Mirzah anaweka tena msisitizo katika maneno yafuatayo;

"Na funuo zote hizi ni *kwa hakika aya za Quran tukuf, zinazohadithia habari za nabii Issa na mama yake Mariam….. Na katika maneno ya ufunuo mradi wa Issa na Mariam* ni mimi" *(Kishti-e-Nooh UK.34)*

Kwa hiyo hapo Mirzah anawasisitizia kabisa kuwa "na katika maneno ya ufunuo" huo uliopo katika Barahain-e-Ahmadiyya, unatoa tafsiri halisi ya hiyo Aya ya 3:56 katika Quran, na kwamba anayetajwa kuwa atafishwa na Mwenyezimungu katika Quran akiwa Issa ni Mirzah Gulam mwenyewe na si Eisa (a.s). Sasa ndugu yangu Eng.Kazema, ni kwa nini basi nyie wa-ahmadiyya mnakwepa tafsiri ya nabii wenu iliyomshukia kama funuo katika Barahain-e-Ahmadiyya kuhusu aya hiyo ya Quran, na badala yake mnatunga ideology zenu? Je mnaona aibu au mnakwepa ukweli? Au hamuamini kuwa Mirza Gulam funuo zake ni za kweli?

Ndugu Eng.Kazema, kwa ujumla ninazo hoja nyingi sana ambazo ninaweza kuzitumia kukujibu hoja zako zote, isipokuwa kwa uchache leo niishie hapa, ili nikupe mwanya wa kujitetea, lakini ikibidi ingekuwa bora zaidi tukipanga muda tukakutana kwa ajili ya mjadala tena mbele ya wa-ahmadiyya wasiopungua 20, ili waweze kupata faida, Inshaallah.

Ninaamini hoja hizi pamoja na majibu utakayozijibu kwa pamoja utaziweka katika gazeti la Mapenzi ya Mungu, ili waungwana wapime kwa akili yao, ni zipi pumba ni upi mchele.

Wa-akhir da'awana, w a l - h a m d u l - l i - A l l a h , Rabbil'aalamiin.

Wwahaadha ssalaam.

Na K.Y.A. Bishazo; Bsc. IT

Rais Kikwete ajibu swali

Kutoka uk. 12

magazeti ya *Mtanzania, The African* na *Rai*.

Ni jambo la kutia moyo sana, kuwa nchi yetu sasa inaanza utamaduni mzuri wa kuheshimu utafiti. Pamekuwepo na upungufu mkubwa sana upande huo, wasomi wengi wamekuwa wakifanya utafiti katika nyanja mbalimbali za Kiuchumi, kihistoria, kisiasa lakini kwa bahati mbaya tafiti hizo zimeishia kuliwa mchwa na kutupwa kama takataka. Utamaduni huu utawapa moyo wale ambao wanalithamini na kulipenda taifa hili. Na matarajio yetu makubwa kwamba aliyebuni jina Tanzania atapewa heshima yake ambayo kwa hakika haitakuwa Ihsani, bali haki yake.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Jamad I/Jamad II 1435 AH | April 2014 | Shahadat 1393 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah bin Umarr.a.yakwambaMjumbewaAllahs.a.w. alisema: Mbora miongoni mwa marafiki ni yule aliye mbora wao kwa mwenzake. Na jirani bora mbele ya Allah ndiye anayemtendea vizuri jirani yake. (*Tirmidhi*)

Mwalimu Nyerere na Waahmadiyya

Na Mahmood Hamsin Mubiru - Dar es salaam

Kutoka Toleo lililopita

Kaluta Amri Abedi na Julius Kambarage Nyerere walikuwa darasa moja shule ya wavulana Tabora. Licha ya kuwa ni shule ya watoto wa Machifu, lakini pia ilikuwa ni shule ya vijana waliokuwa na vipaji maalum. Tulipata bahati ya kuzungumza na mmoja wa wanafunzi wa darasa hilo, Bakari Rashidi Kazema aliyetueleza kwamba nafasi ya kwanza darasani humo ilikuwa ni mashindano baina ya watu wawili - Kaluta na kambarage. Huyu akishika nafasi ya kwanza mwingine hakubali anafanya juhudi. Kwa kiwango kikubwa ule utamaduni wa 'fasta bikul khairat' (Shindaneni katika mema) uliongezeka kasi kutokana na vijana hao bongo zao zilikuwa kali. Bila shaka ushindani huu mkali ulimsaidia Julius kuongeza bidii ya kusoma. Jambo ambalo limekuwa la manufaa kwa maendeleo ya taifa lote.



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere - Rais wa awamu ya kwanza

Tumekwisha ona ari ya kupenda kusoma na kutafakari aliyoiwasha Sheikh Mubaraka Ahmad alipokuwa anafundisha Tabora, moto huo uliendelea miaka mingi baina ya Julius na Kaluta. Julius alikiri kadamnasi miaka mingi baadae ya kwamba alikuwa na malumbano kuhusu dini na kila mara Kaluta alitoa ushahidi na kazi ya Julius ilikuwa ni kuhamaki. Huku akitabasamu Kaluta alikuwa akimwambia Julius Kambarage Nyerere; "Hasira na kuhamaki sio hoja, jenga hoja". Tukio hili miaka mingi baadae liliweza kuelezwa na Mheshimiwa Rais wa nchi Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wakati akieleza umuhimu wa kujenga hoja bila kutanguliza hasira. Inaonesha Kaluta aliendeleza pale alipokuwa ameachia Sheikh Mubaraka Ahmad, ambae daima alifafanua umuhimu wa kuwa na subira katika malumbano na kutokubali kutawaliwa na jaziba na hamaki.

Katika maisha yake ya kisiasa Nyerere alijitahidi sana kujenga hoja na alijitahidi kuvumilia maoni tofauti na wengine. Uhuru wa mawazo ya wasomi ambao ni dhahiri walikuwa wakipingana nae, wakina *Walter Rodney, Wadada Nabudere, Yash Tandon, Issa Shivji* kwa kuwataja wachache. Katika kipindi cha miaka ya 70 mawazo yao yalitawala chuo kikuu na Nyerere aliweza kuwavumilia na mara nyingi alikuwa akienda pia chuo kikuu kusikiliza hoja walizokuwa wanajenga katika mihadhara yao. Ni dhahiri kwamba katika nchi nyingine wahadhiri wa namna hiyo wanaokwenda kinyume na maoni ya kiongozi hupewa chamtema kuni. Kwa mfano Profesa Ali Mazrui alipokuwa chuo kikuu cha Makerere alipewa msukosuko mkubwa na Rais Milton Obote wa Uganda.

-

=Itaendelea toleo lijalo=

Rais Kikwete ajibu swali *'Nani aliyebuni jina Tanzania?'*

Na mwandishi wetu

Swali lililowasumbua wanahistoria wengi ndani na nje ya nchi, la *Nani aliyebuni jina Tanzania*? Limepewa jibu na rais wa Jamhuri ya Muungano Rais Jakaya Mrisho kikwete kwenye siku adhimu ya kusherehekea miaka 50 toka nchi mbili hizi ziungane yaani Tanganyika na Zanzibar. Na huu ukiwa ndio muungano pekee wa nchi za kiafrika kuungana na kudumu kwa amani na usalama kwa nusu karne.

Akihutubia taifa katika sherehe hizo za kufikisha nusu karne, toka nchi hizi mbili ziungane, rais Kikwete ametegua kitendawili ambacho kilikuwa kinawatasa wengi. Bila kuuma uma maneno rais wa Muungano alisema aliyebuni jina hilo ni *Mohammed Iqbal Dar* kijana wa kitanganyika mwenye asili ya Asia aliyekuwa anasoma shule ya watoto wenye vipaji Mzumbe Morogoro.



Bw. Mohammed Iqbal Dar aliyebuni jina 'Tanzania'

Ingawaje miaka mingi kabla, *Mohammed Iqbal Dar* alijitokeza na kueleza kuwa yeye ndiye aliyebuni jina Tanzania kwa kuonesha ngao, zawadi na vyeti alivyopewa, hata hivyo akina Thomas waliweka masikio yao pamba na kutupilia wazo hilo mbali. Mwanahistoria wa Jumuiyya ya Ahmadiyya alijikita zaidi katika utafiti kwa kusoma magazeti ya miaka ya nyuma, *Mapenzi ya Mungu, Mwafrika, Baraza, Daily News, Nationalist* na kuzungumza na wazee na hatimaye kupata fursa ya kutosha ya kuzungumza na Bwana *Mohammed Iqbal Dar* ambaye alikuwa amefika nchini kutoka Uingereza ili kuhudhuria mkutano wa mwaka wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya ambao hufanyika kila mwaka nchini.

Mazungumzo hayo na utafiti uliofanywa viliondoa mashaka yote yaliyokuwa yanajitokeza na hatimaye kuandikwa kitabu alichokipa anuwani ya *'Nani Aliyebuni jina Tanzania'*. Kitabu hiki kilisambazwa sehemu nyingi na kama ilivyo ada wengi wakakikebehi na wakaonesha ya kwamba hakikuwa na lolote la msingi. Hata hivyo magazeti mengi nchini yaliweza kuandika makala nyingi juu ya ubunifu huo wa Mohammed Iqbal Dar. Hayo yote hata hivyo hayakusaidia hata kidogo. Hatuna uhakika sana iwapo Rais alikisoma kitabu hicho, ingawaje muandishi aliwahi kumpatia Bw. Salva Rweyemamu ambaye wakati ule alikuwa mhariri wa

Endelea uk. 11